# Kongamano Pamoja Na Mungu

Asante, Ndugu Orman. Asante sana. Vema, tuna furaha kurudi maskanini tena asubuhi ya leo. Ki—kidogo tu nimepwelewa na sauti; tumekuwa na wakati mzuri sana juma hili. Hili limekuwa juma kuu sana la baraka kwangu. Nami nina hakika limekuwa hivyo kwenu, pia, wengi wenu hapa. Wengi wamempokea Roho Mtakatifu. Hilo lilikuwa ndilo kusudi letu kwenye mkutano huu. Na sababu ya sisi kutoutangaza, kwa mbali, ilikuwa ni kwa sababu ya—ya ukosefu wa mahali pa kuwaweka watu. Mnaona? Tunaninii tu. . . Usiku baada ya usiku, watu wanaondoka tu, hao ni watu wetu wa mahali hapa. Nasi tuliutaja tu miongoni mwa watu wetu hapa.

2 Na kuhusu mchango sasa hivi wa vile vikapu, huo ulikusudiwa kwa watu wetu wa mahali hapa. Jinsi. . . Hilo ni jambo letu la kanisa. Hii ni shule yetu ya kawaida ya Jumapili. Mnaona? Nao. . . Hakika, kama mtu yeyote alitaka kusaidia kwa njia hiyo, tuta—tutahakikisha ya kwamba yamepelekewa wahitaji. Tunazo familia, humu mjini, zisizo na chochote, hawatakuwa na chochote kwa ajili ya Krismasi. Wanalitegemea kanisa hili. Na kwa hiyo, kwa njia hiyo, mbona, yata—yatatumiwa kwa kusudi hilo. Mmoja wa mashemasi, atawaambia ni ya nini, ama dada yangu kule nyuma atayachukua.

3 Sasa, nasikia tayari tumekuwa na ibada ya ubatizo asubuhi ya leo. Kidogo walinitangulia kwa hiyo, sivyo? Vema, basi, tutakuwa tu na nyingine, usiku wa leo, kwa hiyo, basi, tuwe nazo mbili. Kwa hiyo tunadhani. . . Ama, angalau, kidimbwi kitajazwa, kwa kuwa mara baada ya ibada, usiku wa leo, kutakuwako na ibada nyingine ya ubatizo.

4 Na baadhi yao, wao walisema, itawabidi wabatizwe. Kwa hiyo Billy alikuja mbio, dakika chache zilizopita, na kuniambia, kasema, "Usije sasa hivi, kwa sababu ilimbidi Ndugu Neville kubatiza, kwanza." Kisha kasema, "Kuna watu wengi kule waliopaswa kuondoka, mara moja. Wala hawakuwa na hakika ya kwamba tutakuwa na ibada ya ubatizo asubuhi ya leo."

5 Kumbukeni, kidimbwi hiki sikuzote kimefunguliwa. Sikuzote, wakati wowote, saa yoyote ya mchana ama usiku, tayari kwa ajili ya ubatizo. Wahudumu wengine huja humu ndani, wanakitumia kidimbwi hiki kwa kubatizia, kwa hiyo tuna furaha sana kwa ajili ya hilo.

6 Hapa wakati fulani uliopita, kanisa la Methodisti la Park, nilikuwa huko kwa ajili ya hu—huduma ya ibada ya mahubiri. Ndipo huyo ndugu mpendwa akasema, "Nilikuwa huko kwa Ndugu Branham hivi majuzi, kutumia kile—kile. . . " Kasema, "Mnakiitaje kitu hicho?"

7 Nikasema, "Ingekuwa ni vigumu kwa Mmethodisti kusema, 'Mahali pa kubatizia.'" Walikuwa na bakuli dogo pale, wanamonyunyizia, mwajua, kitu kidogo tu kimewekwa juu hapo. Nikasema, "Ni neno gumu kupita kiasi kwa Mmethodisti kusema, 'Mahali pa kubatizia,'" nikasema.

8 Akasema, "Tungependa kuwa na moja ya hizo huku. Kidogo ninaamini katika hilo."

9 Kwa hiyo, kumbukeni, Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, mtu yeyote anayetaka kukitumia, hicho hapo. Ni wazi, maji ni bure.

10 Nasi tuna ufito mdogo, mdogo wenye joto tunaoingiza mle, kujaribu kuyapasha moto. Lakini, ninawaambia sasa, hauyapashi moto. Hayo ndiyo maji baridi kuliko yote niliyowahi kuhisi maishani mwangu. Nami nilibatiza, mara nyingi, ambapo ingenilazimu kuuchukua mguu wangu na kupiga teke barafu kuelekea juu ya kijito, namna *hiyo*, nipate kuwabatiza. Kisha niende nyumbani kwa miguu, nijaribu kwenda ambako ilinibidi kukaa, kubadilisha nguo zangu. Nazo nguo zangu zingeganda mwilini mwangu, nikitembea. Ilikuwa ni vigumu kwangu kupiga hatua, mguu wa suruali yangu ulikuwa umekuwa mgumu kabisa, nikipiga hatua. Wala hayakuwa baridi kama haya. Hayo ndiyo maji baridi kuliko yote niliyowahi kuona maishani mwangu. Kamwe sijawahi kuona maji yoyote kama hayo.

11 Ndugu Kelley, karibu yanigandishe hata kufa, kila ninapoingia mle ndani. Na kwa hiyo baada. . . [Dada Kelley anasema, "Kama unajisikia vizuri, hayo hayajisikii."—Mh.] Hiyo ni kweli. Unapojisikia vizuri, hayajisikii. Dada Kelley anasema, "Unapojisikia vizuri, hayajisikii."

12 Tuna furaha kwa ajili ya kundi hili la watu wenye furaha, lililochanganyana huku, katika madhehebu yote mbalimbali. Ni watoto wa Mungu tu walioletwa pamoja. Kuna watu humu ndani walio Methodisti, Baptisti, Nazarayo, Pilgrim Holiness, Katoliki, Mashahidi wa Yehova, Sayansi ya Kikristo, Pentekoste, kila kitu kimeletwa pamoja.

13 [Mtu fulani anasema, "Hata na Myahudi."—Mh.] Hata na Myahudi. Bwana asifiwe kwa ajili ya jambo hilo. Asante. Tuna furaha sana kwa ajili ya Myahudi. Naam, bwana. Kama—kama isingalikuwa ni kwa ajili ya Myahudi, sijui tungekuwa wapi. Hiyo ni kweli. Sasa, hilo ni zuri sana.

14 Hivyo ndivyo Mbinguni kutakavyokuwa, kabisa, kwa kuwa Mbinguni kutakuwa ni mkusanyiko wa madhehebu yote

mbalimbali. Na hiyo ndiyo sababu tumeketi pamoja katika mahali pa Kimbinguni.

15 Sasa, Doc, hiyo ilikuwa ni saikolojia kidogo. Najua ilikuwa. Yeye. . .sikuwa karibu nayo vya kutosha. Nikiwa kidogo nimepwelewa na sauti, asubuhi ya leo, itaingia kwenye gia ya pili, baada ya kitambo kidogo, na kuanza, mwajua, nitakapoanza, ninaamini.

16 Sasa, nilipata maswali fulani yaliyokuja jana usiku, kuhusu mkutano bado. Bwana akipenda, nitayajibu upesi sana, usiku wa leo, kabla hatujaanza i—ibada ya kawaida ya kuhubiri, usiku wa leo. Na hivyo basi—hivyo basi hakikisheni mtakuja, usiku wa leo, kama mkiweza. Basi Bwana akipenda, ninataka kuhubiri juu ya somo muhimu sana, la kufungwa kwa uamsho huu usiku wa leo, tujuavyo sisi, isipokuwa Roho Mtakatifu aelekeze mbele zaidi.

17 Wengi wenu, bila shaka, itawabidi kurudi nyumbani mwenu, leo hii, au baada ya ibada hii, labda, asubuhi ya leo. Tunataka kusema tunawathamini, sana. Nasi tunataka kuwatakieni Krismasi yenye furaha na Mwaka Mpya ulio bora zaidi. Mungu awe pamoja nanyi na awape mambo mapya, wingi wa Uzima mpya ambao mnautafuta na kuuonea njaa. Hivyo ndivyo ninavyofanya, mimi mwenyewe, ni kumwonea Mungu njaa zaidi.

18 Kuna maswali mengine mengi. Kuna. . .Nina machache tu chumbani, wakati huo tu, walionipa. Pia ndugu fulani alimpa mwanangu, jana usiku, maswali fulani. Wala sikupata nafasi ya kuyafikia, kwa sababu niliyashindilia tu mfukoni mwangu, na muda ulikuwa umeenda sana.

19 Na baadhi yao yanahusu tena Matha-. . .ama Waebrania 6:4. Ndio kwanza Dada Mammie aseme, dakika chache zilizopita, ya kwamba alifurahia sana kulishika hilo, kwa sababu alikuwa ameuliza swali lile lile, siku moja. Hilo ni jambo la ajabu sana, sana. Lakini nina hakika nyote mlilipata, kile lilichokuwa. Natumaini mlilipata. Si Mkristo aliyejazwa na Roho.

20 Sasa kama utaenda kwenye Waebrania 10, utaona ya kwamba yeye alisema mle ndani, ni tofauti, ndipo anazungumza, ile dhambi isiyosameheka, *kwa* Mkristo, bali hii ni, ama, kwa mtu *aliyejazwa*, lakini huyu ni mtu ambaye ni mwaminio mkwamia mpakani ambaye ameonja tu.

21 Tunao katika makanisa yote. Wanakuja tu kanisani, na, loo, wanathamini yale Bwana afanyayo, bali kamwe hawataingia ndani yake. Wanathamini kumwona mtu fulani ameponywa, bali kamwe hawatafanya jitihada yoyote ya kutoka na kuwaombea wagonjwa, na kutembelea hospitali, ama kufanya jambo fulani lililo jema, mnaona, namna hiyo. Mmewaona wa aina hiyo. Wameonja. Wameona. Kama tu nilivyosema, Wakaini, Wakanani, ama. . .

22 Waisraeli, walipokuwa wakikaribia Kanaani, walienda nusura waingie. Walienda kule, mbali kutosha kupata kionjo

cha matunda kutoka kwenye nchi hiyo, lakini wakasema, "Loo, ha—hatuwezi. Ha—hatuwezi kufanya hivyo." Lakini Yoshua na Kalebu walijua wangeweza kufanya hivyo, kwa sababu walikuwa na ahadi ya Mungu.

23 Na hilo ndilo Paulo alilokuwa akijaribu kuzungumzia, kurejea huko nyuma kwa wale waliofika karibu Naye, karibu sana, lakini hawataweka mkono wao juu Yake, wenyewe. Wanasema tu, "Loo, ni—ninaenda kanisani, hayo makanisa. Ninaenda kwe—kwenye kanisa la utakatifu, kanisa la Kipentekoste. Ninaenda kwenye *hili*."

"Lakini je, umempokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini?"

"Loo, la. Sijafanya hilo bado." Mnaona? Haya basi.

24 Lakini mwaminio halisi hawezi kutulia mpaka atakapoingia ndani Yake. Hana budi kwenda huko kuingia ndani Yake. Mnaona?

25 Kwa namna fulani tu ni m—mkwamia mpakani, sasa, huyo ndiye mtu ambaye Paulo ananena habari zake.

26 Hata hivyo, sasa, asubuhi ya leo, ni Ujumbe wa kawaida wa Injili kwa ajili ya asubuhi ya leo, Bwana akipenda, alinipa sauti ya kutosha.

27 Kwa hiyo nafikiri hayo ndiyo matangazo. Sina uhakika, lakini nafikiri hayo ndiyo, nijuavyo mimi. Naye Ndugu Neville amefanya hayo mengine.

28 Nami ninawatakeni ninyi nyote mjue, kama kamwe mkipata kuwa huku. . . Ninyi ambao inawabidi kwenda nyumbani, sasa, wala hamwezi kukaa kwa ajili ya ibada ya jioni, ninawatakeni mjue. Kama mkipata kuwa karibu na hapa, wakati wowote, laiti ingalikuwa hivyo, mpitie hapa na kumsikia mchungaji wetu. Tunaye mchungaji halisi kwenye maskani hii, Ndugu Orman Neville. Sisemi hivyo kwa sababu yeye ameketi hapa. Nimemjua kwa miaka kadhaa. Naye kamwe hajabadilika hata kidogo. Angali ni Orman Neville, mtumishi wa Bwana. Mnaweza kumtegemea. Mtiifu tu, mwaminifu, mhubiri mzuri sana. Mimi huketi kule nyuma. . .

29 Nami nimewasikia wahubiri, kote ulimwenguni, wakihubiri. Lakini wakati mwingine yeye huhubiri mambo ambayo hunistaajabisha, nawaambia, yeye anakuchukua tu, katika—katika mambo hayo madogo anayotumia. Nawaambia, kila ninapokuja, ninaleta. . . ninapata kama masomo kumi na matano kutoka kwenye mahubiri yake, wakati ni—wakati ninapokuja, nikiyaandika. Kwenda nyumbani, "Loo, jamani, hilo si lingefanya ujumbe! Loo, jamani, hilo si lingefanya ujumbe!" Na kuliandika tu chini.

30 Kwa hiyo njoni huku na kumsikia Ndugu yetu Neville, na mshirikiane na watu wetu. Ni watu maskini, maskini kabisa. Ila wanampenda Bwana, nao watawapenda. Na kwa hiyo tuna

furaha mlikuwa pamoja nasi, na tunaomba kwamba Mungu atawabariki.

31 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo kabla hatujaliendea Neno.

32 Bwana mwenye rehema, tunakuja sasa kwa uchaji tu tujuavyo kuja. Tunakuja katika Jina la Yesu, tukiamini ya kwamba Wewe umetuahidi sisi, kupitia Kwake, ya kwamba ungesikia lolote ambalo tungekuomba katika Jina Lake. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utafanya huku kuwe ni kuzuriwa kwetu hapa asubuhi ya leo.

33 Tunataka kukushukuru kutoka kwenye kilindi cha moyo wetu, kwa yale ambayo umetufanyia juma hili lililopita. Mioyo mingi yenye huzuni imefurahishwa. Wengi wa watu wamefanywa kushangilia. Na wengi waliochanganyikiwa, katika Neno, sasa wanapiga makelele ya ushindi kupitia kwa Yesu Kristo. Tunakushukuru kwa ajili ya mambo haya.

34 Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba leo hii itakuwa ni wakati mwingine ambapo utawatembelea watu Wako. Nasi tumekusanyika hapa, sote, aina nyingi mbalimbali, ningesema, za makanisa ya kimadhehebu. Baadhi yao wakiwa na imani tofauti, za labda ubishi wa kirafiki juu ya Maandiko, bali bila kufanya hilo liwe ni kizuizi, hata kidogo, hata kwa dada Myahudi aliyeinua mkono wake. Tumekusanyika katika mahali pa Kimbinguni katika Kristo Yesu.

35 Tunaomba, leo hii, ya kwamba Roho Wako atamwagwa upya juu yetu. Tupe ubatizo mpya, asubuhi ya leo, Bwana, ama kujazwa upya. Nasi tunaomba ya kwamba utawaponya wagonjwa, wanaoteseka, wale walio wahitaji. Huyu hapa mtu anayeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu, wengine wako huko nje, labda, wakiwa na ugonjwa wa moyo, wengine wakiwa na kansa. Wanakufa, Bwana. Nao madaktari wa thamani wa nchi yetu wamebaini magonjwa yao na kuingia kwenye kilindi chake wawezavyo, na labda pamoja na upasuaji, na bado ibilisi huyo anashikilia. Ameyakinia kuyachukua maisha yao. Naye ananinii . . . Wanaweza kukata mahali fulani kwa kisu chao na mikono yao myepesi, kujaribu kumsaidia mtu huyo, lakini pepo huyo ataponyoka aingie kwenye kona nyingine na hapo aibuke tena. Kwa kuwa anaweza vizuri sana kujificha kutoka kwa daktari. Lakini, Mungu, hawezi kujificha kutoka Kwako. Unajua mahali alipo hasa. Basi kwa Neno la imani Yako na Nguvu, itamlazimu kuondoka. Nasi tunakuomba Wewe, leo hii, Mungu, ya kwamba utakifanya kila kitu kibaya kiwaondokee hawa watu, kusudi wapate afya, na kuzifurahia baraka za Bwana Mungu wetu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

36 Sasa, kuna leso nyingi zilizowekwa hapa. Nasi tutaziombea. Na endapo huna moja hapa, nawe unataka moja, vema, tuandikie tu hapa kwenye sanduku la posta tatu mbili tano, na

mara tutaituma moja kwa moja kwako. Hilo linapatikana sasa katika Kitabu cha Waebrania, katika Kitabu cha—cha Matendo, mlango wa 19, ambapo sisi huchukua leso ama nguo kutoka kwa watu, kuziombea.

37 Hebu tufungue, asubuhi ya leo sasa, katika Maandiko, kwenye Kitabu cha Isaya, mlango wa kwanza. Isaya 1, wakati tukisoma sehemu ya Maandiko.

38 Basi wakati mkifungua Kitabu hiki, kutufuatilia katika kusoma, tunataka kuzungumzia jambo fulani kuhusu ibada ya uponyaji inayokuja.

39 Sasa, hatujaribu kusema ya kwamba tunaufanya uponyaji wa Kiungu, hapa, jambo kuu, kwa sababu uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo. Wala huwezi kulifanya kubwa jambo dogo. Bali tunaamini ya kwamba huduma ya Yesu Kristo, asilimia themanini na sita yake, ilikuwa ni uponyaji wa Kiungu. Na katika kuushika usikivu wa watu kwa uponyaji wa Kiungu, kulisababisha utambuzi kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Na wao . . .

40 Yeye alisema, "Ikiwa hamwezi kuniamini Mimi kuwa hivyo, basi ziaminini kazi nizifanyazo. Kwa kuwa nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizitenda kazi za Baba, wala hamwezi kuniamini Mimi, basi aminini hizo kazi."

41 Mnaona, kama Mwanadamu, Yeye alijifanya Mwenyewe Mungu. Msalabani, ama, kabla tu ya msalaba, walimwambia, "Hatukupigi mawe kwa kazi nzuri ambazo umefanya. Bali tunakupiga mawe kwa sababu Wewe ni mwanadamu, ukijifanya Mwenyewe Mungu." Yeye alikuwa ni Mungu. Alikuwa. Mungu alikuwa ndani Yake. Na kwa hiyo, basi, Yeye alisema, "Ikiwa hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo." Mnaona? "Ziaminini tu hizo kazi, kwamba ni za Mungu."

42 Vema, sasa, jambo lile lile liko leo hii. Hakuna mtu duniani ambaye ni Mungu. Bila shaka hakuna. Sisi sote ni wanadamu, kila mmoja alizaliwa katika dhambi, akaumbika katika maovu, akaja ulimwenguni akisema uongo. Lakini kama vile tumelipitia kwa udhahiri sana juma hili, kuonyesha ya kwamba Mungu wakati mmoja aliishi *juu* ya kiumbe Chake, kwa sababu ya dhambi. Kisha akaishi *pamoja* na kiumbe Chake, katika mfano wa mwili, Yesu Kristo; akaweka hema Yake pamoja nasi, akakaa pamoja nasi, "akafanyika mwili," pamoja nasi, apate kuonja dhambi na uchungu, maumivu makali, na mambo tufanyayo. Ndipo akalitakasa Kanisa apate kuishi *ndani* yake. Kwa hiyo ilikuwa ni Mungu juu yetu; Mungu pamoja nasi; Mungu ndani yetu.

43 Yesu alisema, "Katika siku hiyo, mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Nanyi mnaona pale, ni Mungu akifanya kazi

kote. Kwa hivyo, wakati mtu amejisalimisha kabisa kwa Roho Mtakatifu, na kunena, sio huyo mtu anayenena.

44 Ninajua hilo kwa ujuzi. Juu ya ujuzi wangu kidogo pamoja na Kristo, niliona nyakati ambazo—ambazo Yeye angeniruhusu kujitolea Kwake, mpaka sikujua nilichokuwa nikisema. Wala nisingesema hilo, kwa chochote ulimwenguni, bali Yeye alilisema.

45 Hattie anayeketi pale nyuma, huyo mama. Hivi majuzi, wakati huduma hii mpya, ambayo ninatumaini itaingia asubuhi ya leo. Nanyi nyote mmesikia habari zake. Basi wakati tulipokuwa tumeketi. . .Na kuna angalau wanane ama kumi, papa hapa sasa, waliokuwapo wameketi wakati huo. Na basi wakati Roho Mtakatifu alipomgeukia mwanamke huyo na kumwambia aombe chochote alichotaka, naye angepewa. Mnafikiri ningalisema hivyo? Kama ningaliweza, ningelisema sasa hivi. Lakini nisingeweza kusema hivyo. Nami nikatetemeka, nilikuwa dhaifu sana. Ndugu Banks Wood, anayesimama pale, alikuwa ameketi karibu nami. Na jasho likatiririka kutoka mikononi mwangu, nami nilikuwa dhaifu sana hata nikasimama nikatoka nje ya nyumba. Lilinitisha sana. Lakini mwanamke huyo akaomba moja ya mambo makuu sana ambayo mtu yeyote angaliweza kuomba, na akalipokea. Mnaona, huyo alikuwa ni Mungu. Huyo hakuwa ni mwanadamu. Wanadamu hawawezi kufanya mambo hayo.

Yesu aliuambia ule mti: "Mtu asile kutoka kwako."

46 Nao wale wanafunzi, kesho yake. . .Upesi vipi, lilianza kutenda kazi papo hapo. Kesho yake, ulikuwa umeanza kunyauka. Nao wakasema, "Tazama jinsi huo mti umenyauka upesi."

47 Naye akasema, "Mwaminini Mungu. Kwa kuwa amin nawaambia, kama ninyi. . . " Si kama "Mimi," bali kama "ninyi." "Yeyote atakayeuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala asitie shaka, bali aamini yale wamesema yatatimia, uliyoyasema yatakuwa yako."

48 Huyo ni Mungu ndani yako. Unaona? Ni nani anayeweza kuuhamisha mlima ila Mungu? Ni nani angaliweza kuyafanya mambo kutimia namna hiyo ila Mungu? Kwa hiyo, mnaona, pasipo na ubishi wowote, Mungu yuko ndani ya watu Wake. Basi inatupasa kuheshimiana. Inatupasa kupendana. Kupita vizuizi vyetu vya kimadhehebu, tunapaswa kupendana, kwa vyovyote vile. Haidhuru kama hatuwezi kukubaliana.

49 Labda, mitume, wasingeweza kukubaliana. Walitaka kujua ni nani atakayekuwa mkubwa kuliko wote, na mambo mengi. Yohana Marko, na—na Paulo, pale, walikuwa na. . .Na Petro na Paulo walibishana. Lakini, vifungo vya upendo, hivyo ndivyo tunavyojaribu kushindania leo hii, ili kwamba Methodisti wote, Baptisti, Presbiteri, Lutheri, chochote kile, sote tuko pamoja,

kama umoja wa Kikristo. Sasa tunajaribu kujazwa kwa Roho, kusonga karibu zaidi na Mungu. Hilo ndilo ono.

50 Sasa mmepata Isaya 1? Hebu tuanzie kwenye kifungu cha 14. Nami nitachukua somo, Bwana akipenda, kutoka kwenye kifungu cha 18, nipate muktadha wangu.

> *Sikukuu zenu za mwezi mpya na karamu zenu zilizoamriwa, nafsi yangu yazichukia, mambo hayo yanilemea; nimechoka kuyachukua.*
>
> *Nanyi mkunjuapo mikono yenu, nitaficha macho* yangu *nisiwaone: naam, mwombapo maombi* yoyote, *sitasikia; mikono yenu imejaa damu.*
>
> *Jiosheni, jitakaseni; ondoeni* uovu, *uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho* yangu*; acheni kutenda mabaya.*
>
> *Jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu, wasaidieni walioonewa, mpatieni yatima haki yake, wateteeni* wajane.
>
> *Haya, njoni, tusemezane; asema* BWANA*: Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa. . .nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.*
>
> *Kama mkikubali na kutii, mtakula mema ya nchi:*
>
> *Bali kama mkikataa na kuasi, mtaangamizwa kwa upanga, maana kinywa cha* BWANA *kimenena haya.*

51 Mnajua, hivi majuzi, tumesikia mengi sana juu ya makongamano, watu wakikutana pamoja. Hilo ndilo Mungu analozungumzia hapa, kongamano pamoja na watu Wake. "Njoni, tusemezane." Hivyo ndivyo tumekuwa tukifanya siku hizi chache zilizopita. Na mengi sana ya hili taifa, na mambo ya kitaifa siku hizi, yana msingi wake katika makongamano.

52 Hapa siku moja, ninaweza kulikumbuka kwa urahisi, na wengi wa hawa watu wanaweza kukumbuka, lile Kongamano la Wakuu Wanne. Waliwaleta viongozi wanne wakuu wa ulimwengu pamoja, wa ulimwengu unaopenda amani, nao wakafanya kongamano. Na katika kongamano hili walijaribu kuamua jambo lililo bora sana kufanya.

53 Halafu basi tulikuwa na lile Kongamano la Geneva hivi majuzi, ambapo, huko Geneva, watu wa ulimwenguni wanaopenda amani walikusanyika pamoja, kuulizana, na kushauriana, kuhusu amani ya ulimwengu. Hilo liliitwa Kongamano la Geneva.

54 Halafu, kama sijakosea, walikuwa na Ko—Kongamano la Paris, hapa sasa, wakati fulani uliopita. Nao wote wakakusanyika huko Paris, kujadili mizozo, kujaribu kuleta amani.

55 Na sasa Rais wetu mpendwa, Dwight Eisenhower, anafanya ziara ya ulimwengu huru. Magazeti yamejaa hayo. Na redio, juu ya mazungumzo ya Bw. Eisenhower pamoja na watu huru wa ulimwengu, kongamano baada ya kongamano, yeye anajaribu ku—kuhudhuria. Na ninii...Wanasema, katika magazeti, kuhusu jinsi ambavyo ana—ambavyo anakaribishwa mahali pengi sana, na jinsi wanavyouimba wimbo wa Marekani, ama kuinua bendera juu, ama kuinua bendera, hasa, juu, wakati anapokuja. Na—na watu mbalimbali wanampa zawadi, na kadhalika. Ni watu ambao ni wa mataifa yanayopenda amani.

56 Nami nafikiri kwamba inatupasa kumwombea Bw. Eisenhower, wakati wanapoweka juhudi zao zote, kujaribu kuiweka nchi hii ambapo tunaweza kufanya mikutano kama hii, kuwa huru.

57 Marekani, katika dhambi zake zote na shida zake zote, ingali ndiyo bora zaidi ulimwengu uliyo nayo. Ninaamini hivyo. Na Mungu aisaidie kuwa, na sikuzote ibaki jinsi hiyo, kwa kuwa tuna kanuni nzuri sana. Ambapo, maskini ulimwengu huu umeloweshwa damu, kuzihifadhi kanuni hizi.

58 Kwa hiyo nafikiri inatupasa kuomba, wakati wote, ya kwamba Mungu atakuwa pamoja na Bw. Eisenhower, mzee nayo afya yake sio nzuri sana. Na—naye mtu huyo katika hadhi yake, na kutoa hotuba, na akijaribu sana awezavyo. Hata kama hukubaliani naye, katika siasa, mwombee sasa. Ni taifa lako ndilo lililo hatarini.

59 Makongamano yanafanywa kwa nini? Sababu ya makongamano haya ni nini? Hapana budi pawe na sababu, la sivyo wasingekuwa na makongamano haya. Hawana budi kufikia uamuzi fulani wa yale watakayofanya. Hiyo ndiyo sababu ya kongamano, ni kufanya uamuzi. Watu katika mahali pamoja, na mahali pengine, na nia mbalimbali, na mambo madogo madogo yanaibuka *hapa*, na kitu fulani *huku,* na nyuma *hapa*, ndipo inawabidi kuja pamoja na kufanya kongamano, kisha watoe uamuzi wa yale watakayofanya kulihusu. Na hiyo ndiyo sababu yanafanywa.

60 Kisha baada ya uamuzi, ama kongamano kupangwa, hawana budi kuwa na mahali fulani pa kufanyia kongamano hili. Na kama utaangalia, hilo, sikuzote wanajaribu kupata mahali fulani ambapo panapendeza. Nimekuwa huko Geneva, ambako kulifanyiwa Kongamano la Geneva, huko Paris, na—na mahali mbalimbali ambako makongamano yamefanyiwa. Nimekuwa kwenye lile jengo la U.N. Na, loo, ni pazuri, hasa sana huko Geneva. Halafu basi mle ndani, wao...Ninaamini wanajaribu kuchagua sehemu hizi ili kwamba uvutio...Kuna jambo fulani, ambalo, kama ni patulivu na—na panavutia, panaonekana kuichangamsha roho ya binadamu. Ninaamini hiyo ni kweli.

61 Mara nyingi, kwangu mimi, kupanda mlima, kuangalia kutua kwa jua ama...kunanichangamsha tu, na inaonekana kana kwamba tofauti zangu zote zimetatuliwa. Mahali, mahali, mahali palipochaguliwa ambapo kongamano halina budi kufanyiwa. Halafu inabidi maamuzi yatolewe.

62 Halafu wazo lingine ninalotaka mlipate, ni hili, katika kongamano, kwamba hawafanyi kongamano kamwe isipokuwa kuna haja muhimu sana. Ni kwenye wa—wakati mgumu sana, wakati makongamano hufanywa.

63 Kwenye wakati wa mkutano wa wale Wakuu Wanne, lilikuwa ni kongamano kwa sababu Vita vya II vya Dunia vilikuwa karibu vimeshindikana. Basi iliwabidi kukusanyika na kuweka mbinu zao zote pamoja, na kufanya jambo fulani; Bw. Churchill, na Roosevelt, na wengineo. Wakijaribu kuweka akili zao pamoja, kuzileta pamoja, waone yaliyo bora kabisa, kwa sababu ulikuwa ni wakati muhimu sana. Ulikuwa ni wakati ambapo ulimwengu wote ulio huru ungalilipuka. Naye Hitler, siku hizi, angalikuwa mtawala wa kimabavu wa ulimwengu, basi tusingalikuwa na mkutano huu leo hii.

64 Hiyo ndiyo sababu makongamano yanafanywa, na sa—sababu ya kuyaweka mahali palipochaguliwa, na—na sababu inayowafanya kuwa nayo. Na endapo...Nasi tunalazimika kufanya kongamano. Hivyo ndivyo wanavyokutana. Nayo hayo yamekuwa ni makongamano makubwa. Hapana shaka niani mwangu, wala wakati usingeniruhusu, sauti yangu, kuendelea na kusema juu ya makongamano hayo mengine makuu kote katika wakati, ambayo nimesoma habari zake, katika siku za Farao, na kadhalika. Lakini, makongamano makuu ya mfumo wa ulimwengu huu yamefanywa.

65 Na, halafu, Mungu amefanya makongamano makuu. Ulikuja wakati, katika uchumi mkuu wa Mungu, ambapo ilibidi kongamano lifanywe. Basi la kwanza ninaloweza kukumbuka, kwa ajili ya ulimwengu huu, lilikuwa katika bustani ya Edeni. Wakati, Malaika wa Mungu walikuja Nyumbani, wakilia, wakisema, "Mtoto Wako ameanguka. Alitenda dhambi, naye amevunja amri Zako." Ilibidi jambo fulani litendeke. Kiumbe cha Mungu kilikuwa kimeanguka kutoka kwenye neema, nacho kilistahili utengano wa Milele kutoka Uweponi mwa Mungu wake na Muumba wake.

66 Ulikuwa ni wakati muhimu sana, kwa kuwa Mfalme wa Mbinguni alikuwa amesema, "Siku utakayokula huo, siku hiyo utakufa." Na kuweka matumaini yake katika Mwanawe, Mwanawe alikuwa amevunja amri Yake. Ilibidi jambo fulani lifanywe. Ilikuwa ni kiumbe Chake. Ilikuwa ni kazi ya mkono Wake Mwenyewe. Ulikuwa ni upendo wa moyo Wake, mboni ya jicho Lake. Jambo fulani halina budi kutendeka. Kwa hiyo ilibidi kongamano liitishwe.

67 Mungu alichagua mti fulani katika bustani ya Edeni. Na baada ya Yeye kutupa maskini ngozi za kondoo zilizolowa damu katika ninii...nyuma ya vichaka, Yeye alimwita Adamu na Hawa, na hapo akafanya kongamano, akazungumza na kutoa tiba kwa ajili ya jambo hili la kuchukiza ambalo watoto Wake walikuwa wamefanya, kongamano la Mungu.

68 Basi palifanywa uamuzi. Sikuzote, kwenye kongamano, kuna uamuzi. Naye Mungu alifanya uamuzi, kwamba, kwa sababu kwamba Hawa alikuwa...wakati Yeye alipomweka kwenye kizimba cha shahidi, kwa sababu alikuwa ameondoa uhai ulimwenguni, ingembidi kuleta uhai ulimwenguni. Na kwa Adamu; na kwa yule nyoka; na, bila shaka, huyo akiwa ndiye kiongozi wa jamii, jamii yote chini yake ilianguka pamoja na Adamu.

69 Ndipo ninaweza kukumbuka katika kumbukumbu yangu, kongamano lingine, la nabii mtoro ambaye alikuwa amedhoofika katika maamuzi yake, naye akawazia kazi hiyo ilikuwa ni kubwa kupita kiasi. Naye alikuwa ametoroka na kujiolea mke, kisha akarudi nyikani, naye alikuwa kule kwa muda wa miaka arobaini. Nabii, aliyetiwa mafuta na Mungu, akiwa na agizo kuu; aliyezaliwa ulimwenguni, nabii. Lakini, hata hivyo, kwa tisho lenyewe la kosa alilokuwa amefanya, (kulichukua mikononi mwake mwenyewe badala ya kufuata maagizo ya Mungu, yeye akamwua mtu), na kwenye tishio na hofu ya Farao, akakimbilia nyikani, na humo, akakaa, miaka arobaini.

70 Nao watumwa wa Misri, kazi ilikuwa ni kubwa mno, migongo yao ilikuwa inauma sana, mioyo yao ilikuwa imevunjika sana, mpaka kilio chao kikaja mbele za Mungu, hata akalazimika kufanya kongamano.

71 Kunayo njia ya kulazimisha kongamano. Unaweza kulifanya maishani mwako, shindano la kuamua.

72 Mizigo ya hao watu, na vilio, vilikuwa vikubwa sana, hata Mungu akalazimika kuagiza kongamano. Mungu anapofanya uamuzi, hauna budi kuwa hivyo. Kwa hiyo alikuwa tayari, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alikuwa ameweka mwanadamu katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kwa kusudi la kuwakomboa hao watu. Mambo yote yalipangwa kimbele na Mungu. Jina la mtu huyo lilikuwa ni Musa, mtumishi Wake. Kwa hiyo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Musa alichaguliwa kuwakomboa hao watu.

Naye Musa alikuwa amemkosea Mungu.

73 Hilo linapaswa kutupa imani na ujasiri. Sisi ambao tumemkosea Mungu, tungali tuna matumaini. Tunamkosea, kama kanisa. Tunamkosea, kama watu. Lakini hebu tuitishe kongamano, tulizungumzie pamoja Naye, tuone atakalotwambia, tuone tutafikia uamuzi upi.

74 Naye mtu wa Mungu alikuwa amemkosea, ndipo ikambidi Mungu kuitisha kongamano. Asingeweza kumtumia mtu mwingine yeyote. Alikuwa amemchagua Musa. Kwa hiyo anashuka kwenda nyikani, mahali fulani upande wa nyuma ya jangwa, karibu na Sinai. Basi Yeye akachagua juu ya mlima, na kichaka, mahali fulani. Akawazia, "Nitamleta Musa huku juu. Hapa patakuwa ni mahali pazuri, mbali na kondoo wake, mbali na mke wake, mbali na watoto wake, mbali na watu wote. Nami nitaitisha kongomano pamoja naye."

75 Hapo, wakati aliponena na yule nabii, hatimaye walifikia kwenye lile suala. "Nimesikia kilio cha watu Wangu. Hiyo ndiyo sababu nilikuita, Musa. Nimesikia kilio cha watu Wangu kule chini, nami nimekumbuka ya kwamba nilifanya ahadi ambayo sina budi kutimiza. Sasa ninakutuma huko chini."

76 Musa ali—alishauriana na Mungu. Yeye alikuwa ni mwanadamu. Akasema, "Lakini mimi ni nani? Si—siwezi kuzungumza."

77 Halafu kwenye hili—hili kongamano, Mungu akamwambia Musa, "Ni nani aliyeufanya mdomo wa mwanadamu? Ni nani aliyemfanya mwanadamu kuzungumza? Ni nani aliyemwumba kiziwi? Ni nani aliyemwumba bubu?"

Naye Musa angali alilalamika. Alitaka kuuona utukufu wa Mungu.

78 Naye akasema, "Musa, ukitaka kujua kwamba Mimi ni nani, Mimi ni Mungu anayefanya miujiza. Itupe fimbo yako chini." Nayo ikageuka ikawa nyoka. Kisha Yeye akasema, "Ingiza mkono wako kifuani mwako." Kisha akautoa, nao ulikuwa ukoma. Ndipo alipourudisha tena na kuutoa, ukapona. Kasema, "Unajua Mimi ni nani, Musa? Mimi ni Mungu afanyaye miujiza. Mimi ni Mungu awaponyaye wagonjwa na wanaoteseka. Mimi ni Yehova Mungu."

79 Musa akasema, "Ninauona utukufu Wako. Jambo lingine moja ninalotaka kujua, kabla ya kufungwa kwa kongamano hili. Nitamwambia Farao kwamba nimetumwa na nani?"

Akasema, "Mwambie kwamba 'MIMI NIKO' amekutuma."

80 Si "Niliyekuwako," ama "Nitakayekuwako." Lakini, aliyeko milele, "Yeye yule jana, leo, na hata milele." "MIMI NIKO," *NIKO* ni wakati uliopo, sasa. Linajumuisha wakati wa usoni, uliopo, na—na wakati uliopita, "MIMI NIKO."

"MIMI NIKO amekutuma."

81 Musa alipokea maagizo yake kisha akashuka kwenda Misri. Wakati akitoka, akiwaleta watoto, ulikuja wakati, basi, walipozingirwa. Watu, watu walioitwa watoke, watu waliotengwa na ulimwengu wote! Israeli walikuwa ni watu wa Mungu, maadamu wangali Misri. Mara walipotoka Misri, walikuwa ni kanisa la Mungu. Neno "walioitwa watoke," ama,

*kanisa* linamaanisha "walioitwa watoke." Kwa hiyo walikuwa wameitwa watoke kutoka ulimwengu wote, nao ni kanisa.

82 Hivyo ndivyo ilivyo asubuhi ya leo, wale ambao wameitwa kutoka ulimwenguni, haidhuru wana kibandiko cha dhehebu gani. Kama wameitwa watoke, wametengwa kwa Mungu, nao ni washiriki wa Kanisa Lake kuu.

83 Kwa hiyo watu hawa walikuwa wamejitenga, kwa kutoa damu ya mwana-kondoo, na kwa kupaka da—damu, juu ya mwimo wa mlango. Na hiyo ilipakwa kwa hisopo.

84 Angalieni. Ninawatakeni muone jambo fulani hapa. Ni la kushangaza sana. Musa aliamuru kwamba wachukue hisopo, na kuichovya kwenye damu ya mwana-kondoo na kuipaka juu ya mlango. Ile damu, hakika, iliwakilisha Damu ya Kristo. Hisopo ilikuwa ni gugu la kawaida. Ungeweza kulipata mahali popote, kuchuma tu konzi la magugu.

85 Inaonyesha ya kwamba Damu ni rahisi sana kutumia. Hayo magugu yaliwakilisha imani, imani tu katika Mungu. Haikubidi kwenda mahali pengine. Chukua tu imani ya Mungu na upake Damu moyoni mwako. Useme, "Nimetengwa na mambo ya ulimwengu, kwa sababu, kwa imani, ninaitumia Damu kwenye kisa changu asubuhi ya leo. Nitaponywa, kwa sababu ninaipaka Damu juu ya mwimo wa roho yangu. Kamwe sitaruhusu tashwishi inishike tena, kwa kuwa nitajikinga kwa kujipaka Damu ya Yesu, kwa imani (hisopo yangu), juu ya mlango wangu. Wala hakuna adui atakayeingia ndani. Kamwe sitalishuku Neno la Mungu tena." Hivyo ndivyo lilivyo rahisi.

86 Walikuwa wakienda zao taratibu, wakiisha kutenganishwa, na ni watu walioitwa watoke. Ndipo wakaja kwenye Bahari ya Shamu. Nao iliwabidi kusimama. Wasingeweza kuvuka. Yule jemadari mkuu, Yoshua, ilibidi ainue mkono wake na kupiga baragumu, kusema, "Simameni! Komesheni mwendo! Kuna kizuizi mbele zetu. Tuna milima pande zote mbili. Tuko hapa chini bondeni, na hatuna budi kusimama."

87 Basi wakati Kanisa hilo litakaposimama kamwe, hapo ni wakati Shetani atakapochukua mamlaka. Hatuna budi kwenda, sikuzote na upesi sana, tukienda taratibu kuelekea Sayuni. Kamwe msiache Kanisa la Mungu aliye hai kamwe liwe na hatia ya kusimama.

88 Kwa hiyo wakasimama, ndipo kasema, "Kuna nini hapa?" Mara waliposimama na kupiga mahema yao, na kuanza kupumzika kidogo, wakasikia kishindo cha magurudumu. Na njia pekee ya kuepukia waliyokuwa nayo ilikuwa ni kurudi nyuma. Nalo hili hapa jeshi la Farao linakuja, likiingia kuwazuia, ama kuwazingira.

89 Ninyi askari, mkiijua hiyo mbinu, jinsi ambavyo waliwazingira. Palikuwapo na Bahari ya Shamu mbele zao, labda urefu wa maili mbili ama tatu. Hii hapa milima

mirefu; wasingeweza kuipanda. Wangekuwa kama kondoo, waliotawanyika kule, shabaha kwa kila mpiga upinde. Halafu nyuma yao, kwa sababu walikuwa wamesimama, akaja adui.

90 Inaonyesha jambo hili, marafiki, hata kwenye safari ya leo ya kwenda kwenye Nchi ya ahadi, adui yuko mruko mmoja ama miwili nyuma yetu. Hatuwezi kusimama kwenye uamsho huu. Huu hauwezi kuwa kutoa amri ya kusimama. Endeleeni tu kwenda mbele. Endeleeni. Mna Uwepo wa Roho Mtakatifu pamoja nanyi, ule usiku uliotangulia wa jana, na usiku wa jana. Sasa endeleeni kusonga mwingie katika Hilo. Msitoe amri ya kusimama, kwa kuwa adui yuko karibu nyuma yenu.

91 Na mara amri ya kusimama ilipotolewa, na jeshi la Farao likaonekana, likija kwa mbali; vi—vishindo vya magurudumu ya magari ya farasi, huku mavumbi yakiruka, na makelele ya hao askari. Ni wakati wa jinsi gani! Karibu hao watu waingie wazimu.

92 Ila kulikuwako na mmoja, miongoni mwao, ambaye alijua hapakuwapo na sababu ya kujisumbua. Alikuwa amekuwa na makongamano awali. Alijua kile kilichohitajika kumshika Mungu. Kwa hiyo juu, tutasema, juu ya kile kilima, kwenye mwamba fulani, Musa alijificha kutoka kwa hao watoto wengine wa Israeli, na hapo akafanya kongamano. "Bwana, nimetembea nikafika hapa, bali kizuizi kimetusimamisha. Imetubidi kutoa amri ya kusimama."

93 Kama vile ndugu yetu hapa kwenye kiti cha magurudumu. Kama labda wewe unayeketi hapo ukiwa na kansa, ama na ugonjwa wa moyo, ama kitu fulani unachojua utakufa tu mara moja. Adui amekusimamisha. Amekufanya kusimama. Labda umesimama kabla adui hajakupita. Labda kuna jambo fulani maishani mwako, ambalo limekufanya usimame. Hata liwe nini, ungali una majaliwa ya kongamano. Hebu tulizungumze pamoja Naye. Hebu tufanye jambo fulani kulihusu. Haidhuru adui ni nani, kamwe yeye si mkubwa kupita kiasi kwa Mungu wetu. Tunahitaji kongamano.

94 Kwa hiyo Musa akapanda, nyuma ya mahali fulani, tutasema, na kufanya kongamano pamoja na Mungu. Hakujua la kufanya.

95 Labda wewe hujui la kufanya. Labda wewe ni mwenye dhambi, na umetenda dhambi nyingi sana. Labda ulivuta sigara mpaka huwezi kuzivuta tena, wala huwezi kuachana nazo. Labda umekunywa pombe hata huwezi kuinywa tena, wala huwezi kuiacha. Labda umefikia mahali ambapo umejaa dhambi sana na tamaa mbaya, mpaka inakubidi kumtazama kila mwanamke unayemwona, vibaya. Ama, labda hata umepotosha asili yako mwenyewe. Labda umefika mwisho. Sijali mahali ulipo, Mungu angali yuko tayari kuja kwako, katika kongamano, na kulizungumzia pamoja nawe. Labda umeivuruga nyumba

yako. Labda umemwacha mumeo, ama kumwacha mkeo. Labda umewatoroka watoto wako. Huenda kukawa na mambo mengi katika maisha haya, ambayo adui amekutega na kukuingiza ndani yake, lakini, kumbuka, ndugu yangu, dada, ungali unazo haki za kufanya kongamano na Mungu. Naam, bwana. Lizungumzie pamoja Naye. "Yeye ni msaada upatikanao wakati wa shida."

96 Ndipo tunaona ya kwamba Musa alifanya kongamano. Na labda hili lilikuwa ndilo hilo kongamano, "Ee Kiongozi mkuu wa Israeli, nimefanya haya yote kwa amri Yako. Nime—nimewaongoza watu hawa kama tu vile Wewe ulivyoniambia nifanye. Nimewafunika watu hawa kwa damu. Nimeyashusha mapigo kutoka mbinguni. Nimefanya yote uliyoniambia nifanye. Nasi hapa, tumenaswa. Nifanye nini, Bwana? Sina budi kufanya kongamano hili pamoja Nawe." Na labda akiketi juu ya mwamba, ama akisimama karibu, karibu na ufa wa mwamba, ambapo Musa alikuwa akiomba kwenye mahali fulani hapa, palipochaguliwa, katika wakati huu muhimu sana.

97 Ilibidi jambo fulani lifanywe, la sivyo wangepondwa chini ya magurudumu ya hayo magari ya farasi. Wangesukumiwa mle, kila mtoto wa Kiebrania. Kila mmoja wa hao watoto wachanga angalipasuliwa, vichwa vyao mwambani. Nao mama zao wangalipasuliwa, na ninii zao...na kubakwa, nao baba za—zao wangaliuawa kinyama. Huo ulikuwa ni wakati muhimu sana.

98 Huenda kukawa na namna hiyo hiyo ya wakati muhimu sana, labda sio hivyo tu, bali labda kansa imekushika. Labda ugonjwa mwingine. Labda dhambi imekushika. Nayo itakuponda ikuingize moja kwa moja kwenye kuzimu kwa ibilisi, utengano kutoka kwa Mungu. Fanya kongamano, upesi.

99 Ndipo wakati kongamano hili lilipofanywa, Mungu alisimama juu ya huo mwamba, karibu na Musa. Ndipo akasema, "Rudi huko chini kambini, Musa. Rudi moja kwa moja ulikoanzia. Mimi ni Mungu. Shuka kule chini ukaseme na hao watu, wasonge mbele. Nitatengeneza njia wakati utakapofika wa kutengeneza njia. Mimi ni Mungu atengenezaye njia."

100 Musa, baada ya hilo kongamano kwisha, na kuruhusiwa kutoka Uweponi mwa Mungu, pamoja na agizo la kusonga mbele, alishuka chini na kusema, "Msiogope, Israeli. Simameni imara, leo hii, mzione Nguvu za Mungu wetu. Nendeni kuelekea baharini. Msiondoke kwenye ile amri. Agizo ni, 'Songeni mbele!' Nchi ya ahadi ni mali yetu. Adui huyu aliye njiani mwetu, ametukatilia mbali. Lakini Mungu alisema, 'Songeni mbele!' Endeleeni kusonga."

101 Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi. Mungu anawaita, Naye anataka kuwapa karama baada ya karama, na nguvu baada ya nguvu, na neema baada ya neema. Lakini mnajiundia

dhehebu, basi, "Siwezi kwenda mbele zaidi, kwa sababu kanisa halitaniruhusu." Mnaona? Hakuna mahali pa kusimama katika Mungu, hakuna mahali pa dhehebu. Hakuna mahali pa vigezo fulani vyovyote. Jambo ni kwamba, ni kusonga mbele. Nena Neno la Mungu na usonge mbele. Endelea tu kwenda. Endelea kwenda. Mungu akisema ni kweli, ni kweli. Unalo agizo lako.

102 Kama wakisema, "Vema, nilienda kanisani mwangu, nao wakaniambia sikupaswa kwenda kwenye maskani hiyo. Nimechanganyikiwa kabisa sasa, kuhusu kama inanibidi kuwa na Roho Mtakatifu, ama la."

103 Ahadi hiyo ni yenu. "Ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

104 Ati nini? Nena Neno la Mungu. Mungu alisema hivyo. Songa mbele. Mwangalie adui akitawanyika. Angalia Bahari ya Shamu ikifunguka. Fanya kongamano. Songa mbele. Hakika, itafunguka. Mungu ndiye njia ya kuepukia. Alifanya njia, moja kwa moja hadi kwenye nchi ya ahadi. Chochote kilichoingia njiani Mwake, Yeye alikiondoa njiani. Kama kitu chochote kikiingia njiani mwako, basi fanya kongamano na Mungu. Lizungumzie pamoja Naye, kisha uendelee.

105 Hivyo ndivyo Mungu anavyomwambia Isaya hapa. "Loo, wewe ni mwenye dhambi. Dhambi zako ni nyekundu sana. Kwa nini usije tukasemezane? Kwa nini usije ukalizungumzie pamoja Nami? Neema Yangu imetosha."

Kongamano la Bahari ya Shamu.

106 Miaka mingi iliyopita kulikuwako na kongamano lingine, ningetaka kulizungumzia kwa dakika moja. Huo ulikuwa ni muhula wa Krismasi ambao sasa tunauingia, kama kungekuwako na Krismasi, au la. Lakini kulikuwako na kongamano lililofanyiwa Mbinguni, jinsi mpango huu wa ukombozi ungekuwa. Ndipo ikaamuliwa na Mungu, ya kwamba Yeye angefanyika Mtu, ya kwamba angeshuka na kujitwika laana Yake Mwenyewe juu Yake. Isingekuwa ni haki Kwake kumtuma Malaika. Isingekuwa ni haki Kwake kumtuma mtu mwingine yeyote. Hata kama alikuwa na mvulana, isingekuwa ni haki Kwake kumtuma mvulana Wake.

107 Isingekuwa ni haki kwangu kumfanya Joseph ateseke kwa mambo ya hukumu yangu. Nisingekuwa na haki, katika kufanya hivyo. Kama nilipitisha hukumu yangu, ninataka kuikomboa, jambo pekee ninaloweza kufanya ni kuteseka kwa ajili yake, mimi mwenyewe.

Hiyo ndiyo ishara. Hilo ndilo pigo la mauti kwa Shetani.

108 Sasa, ndugu yangu Mkatoliki, na pia wengi wa Waprotestanti wangu, siwaudhi. Lakini mnapojaribu kumfanya Yesu Mungu mdogo kuliko Mungu, kumfanya Mungu mdogo,

mnaikata miguu Yake, mnamshusha kidogo tu chini ya kichwa cha Mungu na kumfanya Mungu mdogo. Mmekosea sana.

109 Yesu alikuwa ni Mwanadamu. Alijiita Mwenyewe Mwana wa Adamu. Hilo lilikuwa ni pigo la mauti kwa ibilisi.

110 Ibilisi yuko juu, alijijengea ufalme maridadi kuliko ule wa Mikaeli. Kaini, mwanawe, alitaka kufanya madhabahu ya kupendeza, yote kutoka kwa matunda na kadhalika. Mungu haishi katika urembo wa aina hiyo.

111 Lakini, Mungu, apate kupiga dhambi pigo la mauti, angalieni jinsi Yeye alivyokuja. Yeye alichagua kuja kwa namna gani? Kulikuwako na kongamano Mbinguni. "Utashuka namna gani? Utafanya hivyo kwa njia gani, Baba," kasema Malaika.

112 "Nitakuwa mmoja wao. Sheria Yangu ya ukombozi, ni, 'Jamaa wa karibu.' Basi itanibidi kuwa Mwanadamu, Mwenyewe." Hilo ndilo pigo lililomwangusha Shetani. Kuzaliwa! Angeweza kushuka pamoja na Makerubi. Angeweza kushuka kwa ngazi za dhahabu. Kungeweza kuwako na nyimbo zilizoimbwa kote mbinguni, na Yeye angeweza kutembea kwenda duniani, na kufukuza kila kitu. Lakini wakati alipofanya hilo kongamano, Yeye aliamua kuja kama Mtoto mchanga.

113 Katika Isaya 9:6, tunaliona. "Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mwana; na uwezo wa kifalme utakuwa mabegani Mwake; ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele. Nayo enzi Yake haitakuwa na mwisho."

"Hii itakuwa ni ishara kwenu, Mtoto mchanga," sio Mungu, "Mtoto mchanga."

114 Angalieni mahali alipozaliwa. Ilibidi iamuliwe, katika hilo kongamano, mahali atakapozaliwa, kuhakikisha Yeye alikuwa ni Mwanadamu. Alizaliwa katika hori. Alichagua, badala ya—ya mlinzi wa ikulu za pembe za ndovu kumsindikiza, badala ya gwaride la Malaika, badala ya Makerubi wanaobingirika, pamoja na—pamoja na mapambo mazuri ya Mbinguni, Yeye alijisukumiza, akajilaza Mwenyewe horini, juu ya samadi ya wanyama, uchafu na kinyaa cha ulimwengu. Yeye alikuwa ni Mwanadamu. Hakuwa Mungu mdogo. Yeye alikuwa ni Mwanadamu. Alizaliwa kama tunavyozaliwa, kupitia uchafu wa kuzaliwa, akatoka kwenye tumbo la uzazi la mwanamke. Sio Mungu; Mwanadamu! Hakuwa kitu, na, si ajabu, ishara iliyo kuu kuliko zote.

115 Mnaona mikutanoni, ile ishara ya upambanuzi, Uwepo wa Mungu aliye hai. Mnaona ishara kila mahali, Zake. Lakini hebu nikwambie jambo hili, ndugu yangu, dada yangu. Kamwe hapajapata kuwako na ishara, nzuri sana, kama ile ishara ambayo Malaika waliwaambia wale wachungaji, "Mtampata

Yeye horini, amevikwa nguo za kitoto." Mnaweza kuona kile Mungu alicho. Hicho ndicho. Linanishangaza, leo hii.

116 Ni kwa nini uamsho unaweza kuja mjini, wa mwinjilisti mkuu mashuhuri, nao watu wa hadhi za juu wahudhurie, meya wa mji, na watu wote mashuhuri sana, ama waliovalia nadhifu, nao maskini kidogo wanadharauliwa? Nanyi mnazungumza juu ya mhudumu fulani aliyeelimika sana, ambaye anaweza kuzungumza maneno ya ufasaha sana ambayo yanaupendeza ufahamu wenu, pamoja na maneno makubwa ambayo watu maskini wasingeyafahamu kamwe, nanyi nyote mnalitukuza hilo.

117 Hivi hamwoni kwamba Mungu yuko katika unyenyekevu? "Hii itakuwa ndiyo ishara. Mtoto huyo mchanga atavikwa nguo za kitoto, na kulazwa horini, juu ya samadi ya ng'ombe na kondoo." Loo, jamani! Hiyo ni ishara. "Hii itakuwa ishara kwenu. Mtamkuta Mtoto mchanga mle."

118 Mara nyingi, watu wanawazia, "Katika maskini maskani ndogo iliyobomoka, wahubiri fulani ambao karibu hawajui ABC zao, majambazi na wauza pombe haramu, na wowote wale, walioongoka, hawana elimu, nao wanatumia misamiati yao ya kusini kama, 'hasina,' na 'beba,' na 'tote,' na 'tafuta,' kamwe hutampata Mungu huko."

119 Lakini huko ndiko mnapompata, amevikwa nguo za kitoto, unyenyekevu. Mnafikiri linakuja kwa njia kuu fulani. Kama ukitaka kufanya kongamano lako halisi na Mungu, chukua kundi la watu kama hao, kisha mkalizungumzie. Unaweza kuziona kazi za Mungu, jinsi ambavyo hakuchukua mchongaji fulani, mwanasanaa fulani mkuu na chochote kile, na kumtolea hotuba ya kiakili. Bali alichukua kitu ambacho kilikuwa ni bure, akashuka kama tu alivyofanya mara ya kwanza.

120 Mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita, "Endapo upambanuzi huu na uponyaji huu, na kadhalika, ulikuwa ni wa Mungu, ukasisi wa Kikatoliki ungalikuwa nao."

121 Ni kwa nini ule ukuhani wa Kiyahudi haukuwa nao? Haukuzaliwa kwenye ikulu. Ulizaliwa horini. Hakuvikwa mavazi ya ushonaji, bali matambara kutoka mgongoni mwa nira ya maksai. Amelazwa juu ya lundo la samadi; Mwana wa Mungu, maskani ambamo Mungu aliishi. Hivyo ndivyo alivyoamua kuja. Nasi inatubidi kuwa na ukosi uliopinduliwa na makoti yenye mikia, na makanisa makubwa, mazuri na minara ya dhahabu. "Hii itakuwa ishara. Mtamkuta katika nguo za kitoto, amevikwa nguo za kitoto, na kulazwa horini. Hiyo hapo ishara kwenu."

122 Mungu huishi katika unyenyekevu; sio katika madoido, hilo sikuzote limekuwa ni wazo la ibilisi. Mungu huja katika unyenyekevu. "Hiyo itakuwa ni ishara." Sio Mungu mdogo, bali Mwanadamu. Mwanadamu! Alilia kama mtoto mchanga, alipokuwa ni Mtoto mchanga. Alicheza mitaani, kama

mvulana, alipokuwa Mvulana. Alifanya kazi katika karakana ya seremala pamoja na Yusufu, kama Mwanadamu kazini. Alikula aliposhikwa na njaa. Alitoa jasho alipokuwa na joto. Alilia alipokuwa na huzuni. Yeye alikuwa ni Mwanadamu.

123 "Hii itakuwa ishara kwenu. Mungu ataishi pamoja nanyi, katika ninii nyenyekevu . . . " Sio mtu mkuu mno, mwenye kiburi, bali maskini Mtu mpole, asiye na usuli. Ishara! Hilo ni pigo la mauti kwa ibilisi, papo hapo. Hilo ni pigo la mauti kwa kila dhehebu na madoido, na madoido yote na utukufu wa ulimwengu huu. Ni pigo la mauti, ambalo Mungu wa Mbinguni alilichagua apate kupitia huko.

124 Hilo ndilo lililotukia kwenye hilo kongamano. Ilibidi iamuliwe. Hivyo ndivyo alivyochagua kuja. Haikumbidi kuja hivyo. Yeye alikuwa ni Mungu wa Mbinguni, lakini alichagua kuja kama Mtoto mchanga. Alichagua kuja hivyo. Hilo ndilo lililotukia kwenye lile kongamano Mbinguni.

125 Hebu nitaje kongamano lingine moja tu, ama mawili. Hebu nilitaje hili. Kulikuwako na wakati . . . baada ya maisha makamilifu ya miaka thelathini na mitatu na nusu kuishiwa. Mtu aliyetaka kuishi kadiri mimi ninavyotaka kuishi, kadiri wewe unavyotaka kuishi. Mtu ambaye alikuwa na jambo la kuishia, ndugu aliowapenda, watu aliowapenda, kutua kwa jua alikopenda kuona. Kumbukeni, Yesu alikuwa ni Mwanadamu. Mungu alikuwa ndani Yake.

126 Ulikuja wakati, ambapo Roho aliyekuwa akimwongoza Mwana-Kondoo, yule Hua, ilibidi kuwe na kongamano kati ya Mwana-Kondoo na Hua, na Wao wakaandaa mahali pa kulifanyia.

127 Baada ya chakula cha jioni usiku huo, walivuka kijito kidogo, Kidroni, na, ama, mahali fulani, nao wakavuka hicho kijito, wakaingia kwenye bustani iliyoitwa Gethsemane. Ilibidi wawe na kongamano. Ilibidi Mungu pamoja na Kristo walizungumzie. Ilibidi Mwana-Kondoo na Hua waketi pamoja. Ilimbidi Hua kuzungumza na Mwana-Kondoo, na kilikuwa ni kifo cha Mwana-Kondoo.

128 Sasa, wakati walipoketi karibu na mwamba huo, na Malaika wote wakashuka chini kutoka Mbinguni, kusikiliza hili kongamano. Loo! Kulikuwako na Gabrieli, Mikaeli, Pakanga, maelfu wote wao, wameketi kando ya ule mwamba.

129 Yeye akawaambia wanafunzi Wake, wachovu, walikuwa na mikutano mingi mikubwa, walikuwa wamechoka, labda kama mlivyo asubuhi ya leo. Lakini Yeye akasema, "Mtakesha nami tu yapata saa moja? Kwa kuwa inanibidi kwenda huko na kufanya kongamano. Inanibidi kwenda peke Yangu." Ndipo wakati wao . . .

130 Kongamano liliwekwa. Naye Mwana-Kondoo, mdogo, maisha mazuri, kamwe hakuna maisha kama hayo. Kamwe

hapakuwapo, kamwe hapatakuwapo, maisha kama hayo aliyokuwa nayo Mwana-Kondoo. Lakini sasa Baba alisema, "Uko tayari? Upendo Wako kwa ndugu Zako ni mkubwa vya kutosha? Je, upendo Wako kwa ulimwengu huo wenye dhambi ulimozaliwa, unaonuka, hivi unawapenda vya kutosha kuachilia maisha Yako? Unawapenda vya kutosha kupachukua mahali pao, kuzibeba dhambi zao, kwa mauti magumu sana, yaliyo muhimu sana?" Ninyi. . .Hakuna kitu kingaliweza kufa kifo cha namna hiyo ila Yeye.

131 Na katika kongamano hilo, uamuzi kama huo ulifanywa, mpaka Damu ikaanguka kutoka usoni Mwake. Alikuwa na majaribu. Dhambi za ulimwengu zilikuwa juu Yake. Halafu akaangalia usoni mwa Hua, na kusema, "Si mapenzi Yangu, bali mapenzi Yako yafanyike."

132 Loo, tunaweza kuwa na uamuzi huo mioyoni mwetu asubuhi ya leo? Unaweza kuachana na maskini hayo maisha yako, machafu? Uko tayari kuuangalia uso Wake na kusema, "Si mapenzi yangu"? "Mimi ni mlevi, bali sitakunywa pombe tena. Mimi ni mcheza kamari; sitakunywa pombe tena. Mimi ni mtovu wa uadilifu, bali sitakuwa hivyo tena. Mimi ni mwongo, bali nitauacha leo. Mimi ni mtu mbaya. Lakini katika kongamano hili, asubuhi ya leo, nitauangalia uso Wako, na kuchukua, kama Bwana wangu Yeye aliyenifia, kuifanya njia yangu dhahiri, 'Sio mapenzi yangu; mapenzi Yako.' Kama ikinigharimu nyumba yangu. Kama ikinigharimu mume wangu, mke wangu, baba yangu, mama yangu, ushirika wangu, ufuasi wangu wa kanisa, chochote itakachonigharimu. Katika kongamano hili, asubuhi ya leo, ninasema ninataka Roho Wako Mtakatifu aishi ndani yangu. Nimesikia habari Zake. Ninakutaka Wewe ndani yangu. Sio yangu, bali Yako. Huo ndio uamuzi wangu." Mungu amepaita mahali hapo, si mahali fulani juu ya mnara, mrefu, bali maskini maskani duni iliyo karibu kuporomoka. Tunafanya kongamano.

133 Hebu nizungumze juu ya kongamano moja zaidi hapa, kwa muda kidogo tu. Nyingi zingeweza kufundishwa. Kulikuwako na kongamano baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Jambo fulani ilibidi lifanywe. Walikuwa ni watu waliokuwa na dhana ya kiakili, kwa hiyo kulikuwako na kongamano lingine lililopangwa. Tunalifahamu, katika Biblia, kama Pentekoste.

134 Iliwabidi kufanya kongamano. Na ilibidi jambo fulani lifanywe, kwa kuwa Yesu alisema, "Msihubiri tena. Msiimbe tena. Msitoke nje na kuhudumu tena. Lakini ninataka kongamano pamoja nanyi. Na katika kongamano hili, nitamleta Roho Mtakatifu. Lakini pandeni mwende mjini Yerusalemu, na huko mngojee mpaka nitakaporudi. Inanibidi kwenda Mbinguni, kuwafanya washangilie. Pia inanibidi kupaa juu kwe—kwenye Kiti cha Enzi cha Ukuu," ule mwili, Yesu, "lakini ninaenda. . .Tutakuwa na kongamano Kule juu. Naye Mungu anayeishi ndani Yangu ameahidi ya kwamba ningeweza

kurudi tena, nami nitakuwa ndani yenu; pamoja nanyi, ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari, ulimwengu. Mpaka yote yamekwisha, nitakuwa pamoja nanyi. Na kazi nifanyazo ninyi nanyi mtazifanya."

135 Kwa hiyo hawakujua jinsi watakavyoweza kufanya hivi, kwa hiyo wakaenda kwenye Pentekoste, ndipo mia moja na ishirini wakaenda kwenye chumba cha juu na kufunga mlango, nao wakangojea na wakangojea.

136 Shida yetu, tusipoweza ku—kuzungumza na Mungu katika dakika kumi, tunachoka, magoti yetu yanauma. Tunataka kuondoka. Asipotujibu kulingana tu na yale tunayotaka, jinsi tunavyowazia, tunachukizwa Naye. "Loo, njoni, tusemezane."

137 "Nendeni Pentekoste, ninataka kusemezana nanyi. Nendeni tu kule mkangojee."

138 Siku kumi, walikuwa wameketi, wanasimama, wakiomba, kila kitu, wakiingojea ile ahadi. "Ndipo mara, matokeo ya lile kongamano Mbinguni yakashuka, Roho Mtakatifu, kama upepo mkali ukienda kasi, nao ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi. Wakajazwa kwa Roho Mtakatifu." Nao wakaenda mbele, wakihubiri Neno.

139 Tunapokuwa na makongamano ya ulimwengu, kwa kawaida wana mahali pao palipochaguliwa. Nao wanafanya nini katika kongamano hili? Wanakunywa vinywaji, kokteli. Wanavuta biri na sigara. Wanadanganyana, na wanahadaana, na mazugumzo ya amani ya ulimwengu.

140 Lakini Mungu anapoitisha kongamano, ni kufunga, kujitakasa, maombi, kupokea maagizo, na kusonga mbele. Hilo ndilo kongamano la Mungu. Sio kufanya karamu, bali kufunga. Sio kushiriki katika uchafu, bali kujitenga, kujitakasa na maovu yote, unapoenda mbele za Mungu. Kujitakasa kwa imani, kwa kuchovya hisopo katika Damu na kuusafisha moyo wako, na kutembea mbele za Mungu, kufanya kongamano. Hiyo ndiyo aina ya makongamano wakati unapokutana na Mungu, ndipo Mungu anakupa maagizo. Ndipo unasonga mbele, Yeye anaambatana nawe.

141 Kuna makongamano mengi makuu tungeweza kuwazia. Ila wakati usingeruhusu. Kumekuwako na kongamano hivi karibuni.

142 Kulikuwako na kongamano katika siku za Martin Luther, kwenye yale matengenezo. Mungu alimwita Martin Luther, aende akahubri kuhesabiwa haki, naye akahubiri.

143 Kulikuwako na kongamano lililofanywa katika siku za Wesley, huko Uingereza, kuhubiri utakaso, na kama vile Wesley alivyoshuhudia . . .

144 Nilivaa koti lake, koti la mwisho alilovaa, joho. Nilisimama kwenye mimbara yake ambapo aliwahubiria watu elfu moja mia

tano kila asubuhi saa kumi na moja. Nikapiga magoti humo chumbani na kumshukuru Mungu kwa ajili ya maisha yake, kile chumba chenyewe alimofia. Mle ndani, Roho akiwa juu yangu, niliwazia, "Naam, Wesley alikuwa mkweli."

145 Malaika watakatifu wa Mungu, na Mungu, walifanya kongamano, ya kwamba wakati wa kuhubiri utakaso ulikuwa umewadia, nao wakamchagua Wesley. Naye alikuwa mwaminifu kwake.

146 Ndipo basi ikaja Pentekoste. Ulikuwa ni wakati wa kurudishwa kwa Pentekoste. Kulikuwako na kongamano lililofanywa Mbinguni. "Je, ni wakati wa kumwagwa kwa utimilifu wa Roho?" Naye akashuka, nao wakahubiri juu Yake. Nasi tukaipata, na kumpokea Roho Mtakatifu.

147 Sasa ninaamini ya kwamba tuko kwenye kongamano lingine, hilo ni, Kuja kwa Mwana wa Mungu. Yeye aliwaambia wanafunzi Wake, "Sijui dakika wala saa; hakuna ajuaye, si hata Malaika. Lakini kutakuwako na kongamano siku moja," kwa maneno mengine, "naye Baba ataamua ile saa nitakayorudi." Ninaamini kongamano hilo linaendelea. Maamuzi yanafanywa.

148 Roho Wake anakuja duniani, kwa nguvu sana, hata atasimama kwenye kusanyiko, ayatambue mawazo ya moyo. Kama Biblia ilivyosema, "Neno la Mungu li hai, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, likikata hata mafuta ya mfupa, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo."

149 Wakati Filipo alipokuja na kuongoka, kisha akaenda akamleta Nathanaeli, naye Nathanaeli akaletwa, yule Myahudi, akaletwa mbele za Yesu. Naye alikuwa akimwambia habari Zake, kasema, "Vema, Nathanaeli, mbona, siku chache zilizopita, mzee mvuvi asiye na elimu alikuja Kwake, Naye alijua. Alimwita jina lake, akamwambia kwamba alikuwa ni nani. Hivi hujui, ya kwamba Masihi ambaye nabii wetu alisema angekuja, hivi hutambui ya kwamba huyo Masihi alikuwa awe nabii, Nabii-Mungu? Huyo hapo. Huyo Ndiye."

150 Hapana shaka Nathanaeli alisema, "Siamini hilo. Nitaenda nikajionee Mwenyewe." Lakini wakati alipofika Mbele za Yesu, Yesu alisema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

151 Basi alipofanya hivyo, yeye alisema, "Ulinijua lini, Rabi?"

152 Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona."

Yeye akasema, "Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli."

153 Wakati, yule mwanamke Msamaria, akiwa na waume watano, alimjia. Naye akasema . . . Hapo alipoanza kuchota maji yake, alimwona Myahudi huyu, ameketi. Akasema, "Nipe maji ninywe."

154 Mnaona, Yeye aliona kiu, kama Mwanadamu. Alikuwa ni Mwanadamu. Katika mwili Wake, alikuwa ni Mwanadamu. Katika Roho, alikuwa ni Mungu. "Mungu aliishi katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake."

Kasema, "Nipe maji ninywe."

155 Akasema, "Mbona, si kawaida." Kwa maneno mengine, "Tuna ubaguzi. Hupaswi kuniomba hayo."

Akasema, "Lakini laiti ungalijua ulikuwa ukizungumza na Nani."

156 Loo, nashangaa, asubuhi ya leo, kama tunajua ni kitu gani kilicho humu chumbani. Laiti tungalijua ya kwamba Roho Mtakatifu, Mwenyewe, Yule atakayeshuhudia kwa niaba yetu ama dhidi yetu, kwenye Siku ya Hukumu, yuko mumu humu chumbani, na anayajua mawazo yetu.

157 "Kama ulijua tu ni Nani aliyekuwa akisema nawe, ungeniomba Mimi maji unywe."

Akasema, "Kisima ni kirefu."

158 Aliendelea kuzungumza naye mpaka akashika roho yake. Ndipo akasema, "Nenda kamwite mume wako mje naye hapa."

Akasema, "Sina yeyote."

159 Kasema, "Umesema kweli. Umekuwa na watano, naye yule unayeishi naye siye mume wako."

160 Akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa tunajua, ajapo Masihi, Yeye atafanya mambo haya. Lakini u Nani Wewe?"

161 Yesu akasema, "Mimi Ndiye." Loo, jamani! "Mimi ninayesema nawe, Ndiye." Mwanadamu tu, akiomba maji anywe, sio kitu kikubwa chenye madoido kutoka Mbinguni. Sio Kiti cha Enzi Cheupe kimewekwa pale, bali Mwanadamu akiomba maji anywe, kutuliza kiu Chake! "Mimi ninayenena nawe Ndiye."

162 Basi akakimbia mjini na kusema, "Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Hiyo siyo ishara ya Masihi? Huyo si ni Yeye?"

163 Mtu Yuyo huyo ametabiriwa, pamoja na manabii huko nyuma katika Agano la Kale. Kasema, "Itakuwa ni siku ambayo vinginevyo watajiunga tu na kanisa, na kwenda kanisani na wawe watu wazuri sana. Nao watakuwa na madhehebu na kadhalika. Nayo itakuwa ni siku yenye utusitusi, si giza wala Nuru. Lakini wakati wa jioni, itakuwa Nuru." Hizo nabii hazina budi kutimizwa.

164 Mnakumbuka, jana usiku, kongomano letu Mbinguni? Mungu alikuwa amewaleta Malaika wote hapo, karibu, kufanya kongamano, ni nani angeweza kulifanya Neno la nabii litimie,

kumleta Eliya...ama ninamaanisha Ahabu huko nje, apate kuuawa.

165 Sasa kuna kongamano linaloendelea Mbinguni. Nuru za jioni ziko hapa. Mabomu ya atomiki na kadhalika yananing'inia kila mahali, nasi tuko kwenye wakati wa mwisho. Makongamano ya ulimwengu yamekwisha. Wakati wa kongamano la Mungu unakuja. Maneno haya hayana budi kutimizwa kwa Mataifa. "Kazi nizifanyazo ninyi nanyi mtazifanya." Wakati umewadia. Kongamano limefanywa. Roho yuko hapa.

166 Sasa, rafiki, katika kufunga, ninasema hivi. Uko kwenye kongamano, asubuhi ya leo. Uko. Nayo kesi yako iko tayari kutetewa. Kisa cha—chako cha maradhi kiko tayari kutetewa mbele za Mungu mwenye rehema. Kesi yako ya dhambi iko tayari kutetewa mbele za Mungu mwenye rehema, na kuwa na hakika ya kwamba unaikubali.

167 Kwa kuwa, hebu nikwambie, nitazungumza juu ya kongamano la mwisho litakalopata kufanywa. Mungu na aturehemu. Ni kitu kimoja tu kitakachosimama kule, kilichopatanishwa. Hiyo ni ile Hukumu. Na jambo pekee utakalopatanishwa nalo, ni wakati umeikubali Damu ya Yesu Kristo, kama msamaha wako, na umejazwa na Roho Wake. Hilo hapo kongamano ambalo kila mwanamume atakabiliwa nalo, kila mwanamke atalikabili, kila mtoto atalikabili. Kuna mahali palipochaguliwa ambapo kongamano hilo litafanyiwa, na kutakuwako na Hukumu kuu ya Kiti Cheupe cha Enzi itakayowekwa. Mungu amewaruhusu manabii Wake kuangalia ndani, na kusema, "Vitabu vilifunguliwa, na Kitabu kingine, ambacho ni Kitabu cha Uzima. Elfu kumi mara elfu kumi ya wahudumu na Malaika wanamhudumia."

168 Halafu, iliandikwa, "Kama mwenye haki akiokoka kwa shida, mwenye dhambi na asiyemcha Mungu ataonekana wapi?"

169 Msimamo wako utakuwa nini kwenye kongamano hilo? Huenda ulikwepa hayo yote, kote katika maisha yako. Huenda ukatoka kwenye mlango huu, asubuhi ya leo, na kuukwepa huu. Lakini, rafiki yangu, kamwe hutaikwepa hiyo. Utakuwa Huko. "Kwa kuwa watu waliwekewa kufa mara moja, lakini baada ya hiyo Hukumu." Kutakuwako na kongamano kuu ambapo sisi sote tutasimama pamoja. Na tutatoa hesabu kwa ajili ya asubuhi hii, kwa ajili ya kongomano hili la duniani ambalo tumefanya asubuhi ya leo.

170 Endapo wewe ni mwenye dhambi, kubali rehema Zake tunapoomba, mnapoviinamisha vichwa vyenu.

171 Kabla tu hatujaomba, nanyi huku mmeviinamisha vichwa vyenu, sijui, asubuhi ya leo, tukiketi kwenye kongomano hili, kama Roho Mtakatifu hajakwambia, "Una hatia."

Na labda unasema, "Roho Mtakatifu, unaona, ni *hivi*."

172 Hivyo ndivyo Musa alivyosema kwenye lile kongamano la Bahari ya Shamu. “Ni hivi, Bwana. Nimekuja umbali huu, bali siwezi kwenda mbali zaidi. Kuna kitu fulani njiani mwangu.”

173 Huenda kukawa na kitu fulani njiani mwako. Lakini, kumbuka, Mungu alimwambia Musa, “Nenda, ukanene na wana wa Israeli, na msonge mbele.”

174 Kama ungetaka kukumbukwa katika maombi, unaweza kuinua mikono yako na kusema, “Niombee, ndugu.” Mungu akubariki. Jamani! Kote jengoni, madazani ya mikono.

175 Baba wa Mbinguni, kwa sauti hii iliyovunjika ambayo kidogo imeharibika, kutokana na kuhubiri, bali kwa namna fulani, nyingine, Roho Mtakatifu mkuu amewapa watu wazo lililokusudiwa. Wakati, nabii alisema, “Njoni sasa, na tusemezane, asema Bwana.”

176 “Sasa njoni, na tufanye kongamano sisi kwa sisi, mumo humo kitini tunamoketi. Nimeketi hapa, karibu nawe. Ninazungumza nawe.”

177 “Lakini, Bwana, nimetenda dhambi,” asema mwenye dhambi. “Nimetenda nyingi sana. Si—siamini ungeweza kunisamehe, Bwana. Mimi ni mlevi. Mimi ni kahaba. Mimi ni, loo, mtu mwenye sifa mbaya. Siamini, Bwana, kungekuwako na nafasi yoyote kwa ajili yangu.”

178 Ndipo tunasikia yale Maneno mazuri yakirudi, “Dhambi zako zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji. Zijapokuwa nyekundu kama bendera; kutoa uhai wa watoto wengi wachanga kabla hawajazaliwa, na—na mambo ambayo yamekuwa ya kuchukiza sana. Zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu za mwana-kondoo.” Ni rehema jinsi gani! “Na tusemezane,” asema Mungu sasa.

Hebu tukutane, tufanye kongamano hili, Bwana.

179 Na—na Wewe unanena na watu Wako. Wanainua mikono yao, ambayo inaonyesha ya kwamba umeketi karibu nao. Kwa kuwa imeandikwa katika Maandiko, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote anipao Baba watakuja Kwangu. Nami nitawapa Uzima wa milele, na kuwafufua katika Siku ya mwisho.”

180 Sasa tujalie, Bwana, ya kwamba kila mmoja aliyeinua mikono yao, na wale ambao hawakuinua mikono yao, popote ambapo makongamano Yako madogo ya kibinafsi yanafanyiwa katika jengo hili sasa hivi, pamoja na hao watu, jalia wakubali neema Yako ya msamaha na kujazwa kwa Roho Wako, na kuoshwa katika Damu Yako. Ndipo mwishoni mwa safari, Wewe unaweza kusema, “Ni vema, mtumishi wangu mwema, mwaminifu. Ulikuwa mwaminifu asubuhi ile, kwenye Barabara ya Nane na Penn, sasa ingia katika furaha za Bwana,

zilizoandaliwa kwa ajili yako tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu."

181 Bwana, Mungu wangu na Baba Yangu, ninawakabidhi Kwako. Siwezi kufanya la zaidi. Mimi ni mhubiri Wako tu, wala siwezi kufanya la zaidi. Hao ni Wako. Tenda nao, Baba, kulingana na mahitaji yao, ya moyo wao. Tunawaruhusu. . . ama kuwakabidhi Kwako, katika Jina la Mwanao, Yesu Kristo. Amina.

182 Kama ulipata kuona, maskanini, siwaruhusu watu kwenda wakawavute watu madhabahuni. Siamini katika jambo hilo. Mungu asipokuleta, haitafaa chochote kwa mtu mwingine kukuleta. "Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu. Na wote ambao Baba. . . " Naye Baba hukuvuta kwa sababu jina lako liko kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. "Na wote alionipa Yeye watakuja Kwangu." Kama uko kitini mwako, madhababuni, popote ulipo, utakuja. Hiyo ni kweli kabisa. Yesu alisema hivyo.

183 Kwa hiyo sasa, ninyi watu wapendwa mlioinua mikono yenu, hatua ifuatayo kwenu kuchukua, endapo hamjabatizwa, ni kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu. Hayo ndiyo maagizo ya daktari, Daktari Simoni Petro, aliyekuwa na zile funguo za Ufalme, na kuwaambia jinsi ya kuingia.

184 Kwenye Siku ya Pentekoste, wao walisema, "Tufanye nini tupate kuokolewa?"

185 Yeye akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu." Hivyo ndivyo mmefanya sasa hivi. "Kisha mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu," kuwaonyesha watu, na ulimwengu, ya kwamba mnaamini (mauti, kuzikwa, kufufuka kwa Yesu Kristo) Yeye alizichukua dhambi zenu. "Kisha mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Fuata agizo hilo.

186 Kama si kwenye maskani hii, kwenye maskani unayohudhuria, kanisa unalohudhuria, popote pale, usikae nje. Nenda moja kwa moja kwenye mwili wa waaminio wa kiroho. Nenda kwenye Assemblies of God, church of God, Umoja wa Kipentekoste, Uwili wa Kipentekoste, Utatu, chochote kile. Sijali uendako, bali nenda upesi kwenye kanisa. Weka ushirika wako mle ndani. Kama wakifundisha mambo madogo madogo, labda, ambayo wewe hufundishi; usiseme, "Vema, Ndugu Branham hakulifundisha namna hiyo." Vema, haileti tofauti yoyote, kwa vyovyote vile. Kama unaye Roho Mtakatifu, endelea. Ungana nao. Endelea. Sote tu—tutakuwa mmoja, kwa vyovyote vile.

187 Wakati hekalu la Sulemani lilipokatwa, kote ulimwenguni, lilikatwa kutoka kote ulimwenguni, mawe mbalimbali yanayoonekana ya kuchekesha, na kila kitu kingine. Lakini yalipoanza kuja pamoja, hapakuwapo na sauti ya msumeno wala sauti ya nyundo. Miaka arobaini katika kule kulijenga lile hekalu, kamwe hawakusikia nyundo moja ikipiga, wala sauti moja ya msumeno. Yote yalikuwa yamekatwa vizuri tu.

188 Makanisa haya yote makuu, yaliyo na Roho Mtakatifu, yataingiana moja kwa moja pamoja katika mahali pao pa kuunganishiwa, kwenye ile Siku, katika Mwili wa Kristo, kwa ajili ya Unyakuo. Kwa hiyo nenda tu mahali wanapoiamini Injili.

189 Sasa, rafiki zangu wa thamani, sikujua kwamba nilikuwa nimechukua kiasi hicho cha muda wenu. Sijui niliingia saa ngapi. Ilikuwa ni saa tatu na nusu ama saa nne, ama kitu fulani? Saa nne. Siwezi . . . Ni hivyo, muda mrefu hivyo kweli? Ni vigumu kwangu kuamini hilo.

190 Tunao wakati tu wa maombi kwa ajili ya wagonjwa. Tuliwaahidi hilo. Sasa, dakika moja tu. Kama mtatupatia tu dakika kumi na tano. Ninii tu . . . Ninaamini ni kasoro dakika kumi na tano, kwa hiyo tuchukue tu dakika hizo kumi na tano kwa saa yangu ya mkono. Sikilizeni. Hakuna kitu . . .

191 Jukumu lako la kwanza, unapokuwa mgonjwa, hakika, unaenda kwa daktari wako. Yeye anafanya yote awezayo kufanya. Endapo hawezi kufanya cha zaidi, unayo haki ya kumwendea yule Mtaalamu mkuu basi. Sasa, hatuwapingi madaktari.

192 Ninao madaktari marafiki wengi wa thamani ambao ni masahibu wangu, watu wazuri wanaomwamini Mungu. Nami huwaombea, na hata wao wananiombea. Hiyo ni kweli. Wao hupata mgonjwa wasiyeweza kumfanyia lolote. Madaktari wengi wazuri, hakika, sitataja jina lao. Labda hawajajazwa na Roho Mtakatifu na kadhalika, bali wao ni watu wazuri. Wanasema, "Ndugu Branham, hakuna kitu ninachoweza kufanya na mgonjwa huyo; naomba umchukue."

193 Ninasema, "Mtume huku. Hebu mimi . . . Siwezi kumponya. Nitamruhusu kwa Yesu, nimkabidhi kwa Yesu Kristo, acha amponye." Mnaona? Kwa hiyo hilo ni sawa.

194 Lakini, angalieni. Kama kuna uponyaji wowote unaotendeka, Kristo atakuwa Ndiye anayeufanya. Daktari anaweza kuondoa kizuizi, kung'oa jino, ama—ama kukatilia mbali mahali pamoja, atoe kidole tumbo, achukue, akatilie mbali kansa, akatilie mbali dutu, ama afanye upasuaji; ama kwa ajili ya kitu kingine, aweke sumu ndani yako, kuua viini. Bali hakuna kitu kinachoweza kuponya ila Mungu, maana inabidi iwe ni uumbaji, kupafanya pakue tena. Wala hakuna dawa itakayoumba. Mnaona? Kunaye Muumba mmoja tu, huyo ni Mungu. Halafu, Zaburi 103, mnaona. Maandiko yote ni ya

kweli. “Mimi ndimi Bwana niyaponyaye magonjwa yenu yote.” Hilo halisemi daktari hana sehemu ndani yake. Naam, anayo. Kama nikivunja mkono wangu, jukumu langu ni kumwendea daktari anayejua jinsi ya kuurekebisha mkono huo, bali hawezi kuuponya mkono huo. Anaweza tu kuurekebisha, airudishe hiyo mifupa mahali pake. Ndipo Mungu anatoa kalisi na kadhalika, na kuumba vitu, humo ndani ya mkono wangu, vinavyoukuza na kuuunganisha tena. Mungu ndiye mponya. Mnaona?

195 Sasa, tumekuwa tukihubiri juma hili. Tabia ya Kiyahudi kwa ajili ya watu, katika wakati wa Kiyahudi, ilikuwa ni kwenda, kuweka mikono juu ya wagonjwa. Hivyo ndivyo walivyofanya. Kila kitu kilikuwa ni kuwekea mikono. Ulikuwa ni utaratibu wa Kiyahudi. Lakini kamwe haikuwa hivyo kwa Mataifa, kamwe. Wakati binti ya Yairo (kuhani wa Kiyahudi), wakati alipokufa, yeye alimwambia Yesu, “Njoo, uweke mikono Yako juu ya mtoto wangu naye ataishi.” Weka mikono Yako juu yake.

196 Lakini wakati alipokwenda kwa akida wa Kirumi, yeye alisema, “Sistahili Wewe kuja nyumbani mwangu. Simama huko nje mahali ulipo, na useme tu Neno.” Alitambua mamlaka ambayo Yesu alikuwa nayo. Akasema, “Mimi ni mtu mwenye mamlaka, nina ninii . . . ” Alikuwa akida. Ilimaanisha—ilimaanisha watu mia moja chini yake. Akasena, “Nikimwambia mtu huyu, ‘Fanya *hili*,’ analifanya. Na mtu yule, ‘Fanya *lile*,’ analifanya.” Akasema, “Nawe una mamlaka juu ya kila ugonjwa, na kila mateso, na kila kitu. Vyote viko chini ya amri Yako. Wewe ni Jemadari mkuu.” Loo, napenda hilo.

197 Hilo hata liliugusa moyo wa Yesu. Naye akageuka basi, kwa Wayahudi, Naye akasema, “Sijapata imani kama hiyo katika Israeli.”

198 Yule mwanamke Msirofoinike, Myunani Mmataifa, alimjia na kusema, “Bwana, nina mtoto anayelala hapa chini, ambaye ibilisi anamsumbua sana.” Labda alikuwa mwenye kifafa ama namna fulani ya wendawazimu. Akasema, “Yuko katika hali mbaya sana. Utamponya?”

199 Naye akaijaribu imani ya mwanamke huyo. “Mbona,” akasema, “si vema kuchukua chakula cha watoto na kuwapa mbwa.” Akimwita mbwa. Na katika siku hizo, mbwa alikuwa ni mmoja wa . . . kitu kama nguruwe mwitu, kitu duni sana kilichokuwako. Kasema, “Si vema Kwangu kuchukua chakula cha watoto, na kuwapa ninyi mbwa.”

200 Akasema, “Hiyo ni kweli, Bwana.” Loo, napenda hilo. “Hiyo ni kweli.” Kasema, “Lakini, unajua, mbwa, chini ya meza, hula makombo ya watoto.” Hilo lilimgusa.

Akasema, kama wewe ulivyofanya hivi majuzi, Hattie, jambo lifaalo.

201 Akageuka akasema, “Kwa neno hili, ibilisi amemwacha binti yako.” Haikumbidi kumwendea na kumwekea mikono.

Kwenye Siku ya Pentekoste, hapo Roho Mtakatifu aliposhuka. . .

202 Filipo alishuka kwenda Samaria. Wao walikuwa ni nusu-Wayahudi, kwa hiyo, aliposhuka, ilibidi kuwawekea mikono, wampokee Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hakuwa ameshuka juu ya yeyote wao, bado, kwa hiyo wakatuma mtu na kumchukua Petro. Walikuwa wamebatizwa katika Jina la Yesu, kwa hiyo wakapanda juu na kuwachukua Petro na Yohana, huko Yerusalemu, kwenye makao makuu. Basi wakashuka na kuwawekea mikono yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Ndipo Petro akapanda juu kwenye nyumba ya Kornelio. . . Mnaona, ilimbidi kuwawekea mikono. Angalieni, Matendo 19, wakati kundi hilo la Wayahudi huko Efeso, ilimbidi kuwawekea mikono, wapate kumpokea Roho Mtakatifu.

203 Lakini, wakati akiwa kwenye nyumba ya Kornelio, "Alipokuwa akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia." Hakuna kuwekewa mikono. Roho Mtakatifu alishuka wakati walipoisikia ile Kweli. Walikuwa na njaa na wakimngojea.

204 Una njaa ya uponyaji hivyo, asubuhi ya leo? Basi hebu Roho Mtakatifu anene, ikiwa Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini hilo? Hivi Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya"? Yeye alijitangazaje Mwenyewe kwa watu, kuwa ni Masihi wao, Masihi wa Wayahudi? Alilifanyaje kwa Wayahudi? Kwa kuwaambia siri ya moyo wao. Walimtambua, Masihi. Ni wangapi wanaojua hilo ni kweli? Hakika.

205 Wakati Petro alipokuja, na Yeye akasema, "Jina lako ni Petro." Tena akasema. . .Ama, "Jina lako ni Kefa." Kasema, "Utaitwa Petro. Jina la baba yako lilikuwa ni Yona." Hilo lilitosha. Yeye alijua huyo alikuwa ni Masihi.

206 Wakati Filipo alipoenda akampata Nathanaeli, Yeye alisema, "Wewe ni. . .Wewe ni mtu mzuri, mwaminifu."

Yeye akasema, "Sasa, Rabi, ulinijua lini Wewe?"

207 Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." Maili kumi na tano kuizunguka milima, safari ya siku moja, "Nilikuona."

Akasema, "Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli."

208 Akaenda huko chini kwa Wasamaria. Alihitaji kupitia kule. Kwa nini? Alishuka kwa Wasamaria. Basi kulikuwako na mwanamke Msamaria, na kwa hiyo akawazia angempa tu ishara ya Masihi. Naye akasema, "Nenda kamwite mumeo mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

Akasema, "Umesema vema, maana unao watano."

209 Akasema, "Bwana," kwa maneno mengine namna hii, "tumekuwa tukimtazamia Masihi kuja, na Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii. Nasi tunajua, Yeye ajapo, atatwambia mambo haya. Kwa hiyo, hapana shaka Wewe ni namna fulani ya nabii."

Akasema, "Mimi ndiye Masihi. Mimi Ndiye unayemzungumzia."

210 Akaacha mtungi huo wa maji, kahaba na aliyekata tamaa, ile hali aliyokuwa nayo, akakimbia mjini, na kuwaambia hao wanaume, "Njoni, mwone Mtu Ambaye aliniambia yale yaliyo moyoni mwangu. Huyo si ndiye Masihi? Si ni Masihi huyo?"

211 Hata wakati mmoja halikufanywa kwa Mataifa. La, bwana. Hii ndiyo siku yao, wakati Nuru za jioni.

212 Wayahudi wako katika taifa sasa, kuutawala ulimwengu. Wakati mmoja waliutawala. Wanarudi. Angalia mtini ukichipuza majani yake, huko ng'ambo. Mwangalieni Myahudi, popote alipo, kalenda ya Mungu, mtakuja kujua. Kamwe Yeye hatawaacha Israeli. Lakini ilibidi Israeli wapofushwe. Sisemi jambo hili kwa niaba ya mwanamke huyu Myahudi anayeketi hapa. Lakini ilibidi Israeli wapofushwe, kusudi tupate nafasi. Wapendeni. Msijali, watachanua tena. "Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu. Yaliyosazwa na madumadu, yameliwa na nzige. Lakini nitarudisha, asema Bwana." Hayo yaliliwa tu, kwa kipindi fulani, tupate kuingizwa. Macho yetu yamefunguliwa.

213 Sasa ni kitu gani? Siku yetu inakwisha. Wayahudi wanaanza kukusanyika tena, pamoja, kama Mungu alivyosema. Nazo Nuru za jioni zinawaka, juu ya nini? Nuru ziko wapi wakati wa jioni? Magharibi. Zilimulika Mashariki, kwa Myahudi, watu wa mashariki, hapo mwanzo. Imekuwa ni siku yenye giza ya madhehebu na kadhalika, lakini Nuru ya jioni itaangaza juu ya Mataifa, bara za Magharibi. Sisi hapa sasa, kwenye mwisho. Tuko—tuko kwenye Pwani ya Magharibi. Kama ungeenda mbele zaidi, unarudi Mashariki tena. Ustaarabu umesafiri hivyo. Kwa hiyo, Nuru za jioni zinawaka, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

Na tuombe.

214 Sasa, Bwana, hawa wote ni Wako. "Neno imani linatokana na kusikia, kusikia Neno la Mungu." Na, Mungu, Wewe unayadhihirisha Maneno Yako, kuwathibitishia watu ya kwamba Wewe ni Mungu. Sasa na ijulikane, asubuhi ya leo, ya kwamba Wewe ni Mungu, nami ni mtumishi Wako, nikiwaambia ukweli wa Uzima wa Milele. Kupitia kwa Yesu Kristo Bwana wetu, tunaomba. Amina.

215 Ninaamini, Billy aliniambia huko nje, ya kwamba kulikuwako na lu—lundo kubwa la kadi za maombi, watu wengi hapa. Hatuwezi kuwaleta wote huku juu, mnajua hilo, ili—ili kuthibitisha hilo, ama kwamba tu mpate kuona. Sasa,

haimbidi Mungu kufanya jambo hili. Na kila mtu anajua jambo hilo?

216 Haikumbidi Yesu kumponya mtu yeyote alipokuwa hapa duniani. Mlijua hilo? Lakini aliwaponya, lipate kutimia lililonenwa na nabii. Hiyo ni kweli?

217 Yeye hufanya hivi, Neno lipate kutimia, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu."

218 Mnaona, walikuwa na Billy Graham na Oral Roberts, hao, katika siku za Sodoma. Watu kama hao walishuka wakaenda kuwahubiria Wasodoma jijini.

219 Lakini mteule Ibrahimu pamoja na kundi lake walikuwa ni kundi lililoitwa litoke, waende upande mmoja. Ni Malaika wa namna gani aliyebaki nyuma na kuwahubiria? Angalieni. Huyo Mtu aliketi pale, akasema alikuwa ni Mgeni kutoka nchi ya kigeni. Mavumbi nguoni Mwake. Alikuwa tu amekula sehemu ya ndama, akanywa maziwa kutoka kwa mama yake, akala ugali wa mahindi, pamoja na Ibrahimu. Wakati, labda alikuwa na mgwisho, akiwafukuza nzi, wakati Yeye alipokuwa akifanya hivyo, ameketi pale, akila. Basi baada ya Yeye kuondoka... Ibrahimu alimwita, "Elohimu, Mwenyezi." Lakini alikuwa ni Mwanadamu; Mungu ndani ya watu Wake. Sasa angalieni kile Yeye alichofanya, jinsi alivyojua. Aliketi pale na kuzungumza na Ibrahimu. Akasema...Sasa, mara ya kwanza aliyokuwa amekutana na Ibrahimu, mara ya kwanza Ibrahimu alipokuwa amemwona, na akijua.

220 Nao hawa watu wengine walikuwa waende Sodoma. Nao wakashuka kule chini na kuhubiri, na kuwapofusha hao watu. Je, hivyo sivyo kuhubiriwa kwa Injili kunavyofanya, kumpofusha asiyeamini? Angalieni.

221 Lakini Huyu alisimama kule nyuma pamoja na Kanisa teule, Ibrahimu na kundi lake, waliotahiriwa, walio halisi. Akasema...

222 Lutu alikuwa yu—yule anayeishi mjini, na yuna wakati mzuri sana. Basi angalia jinsi binti zake walivyokuwa, na jinsi wanawe walivyokuwa, na kila kitu. Hiyo ni kama tu ulimwengu siku hizi, Sodoma, dhambi na kila kitu. Hilo ni kanisa, la kawaida.

223 Lakini Kanisa, la kiroho, ni kundi lililoitwa litoke, lililotengwa. Ni Malaika wa aina gani aliyewajia? Sasa hebu tuangalie hilo. Sasa, kumbukeni, Bwana wenu alisema, "Kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu." Yesu alisema hivyo. "Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatashindwa." Sasa sikilizeni kwa makini, na mtulie.

224 Sasa, Malaika huyu amenena na Ibrahimu. Akasema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" Yeye alijuaje alikuwa ameoa? Alijuaje alikuwa na mke? Pia alijuaje jina lake lilikuwa ni Sara? Ajabu, sivyo?

Naye Ibrahimu akasema, "Yuko hemani, nyuma Yako." Uh-huh.

225 Akasema, "Ibrahimu, kwa kuwa u—unamwamini Mungu, na utakuwa mrithi wa dunia, Mataifa yote na kadhalika wataingizwa katika Ufalme na Uzao wako, na ninii yako. . . hii ahadi imefanywa kwako, sitafanya aha-. . . chochote kufichika kwako, Ibrahimu." Loo, napenda hilo. "Sitakuficha hili, Ibrahimu. Lakini umeniamini Mimi, kwa ajili ya mtoto huyo mchanga, kwa muda wa miaka ishirini na mitano. Sasa una umri wa miaka mia moja, naye ana tisini. Lakini, Ibrahimu, kulingana na wakati wa uhai. . . " Katika kusanyiko lililochanganyikana, mnajua ninalomaanisha, zile siku ishirini na nane. Alikuwa amekoma, miaka hamsini, ama zaidi, naam, miaka sitini kabla ya hapo. Kasema, "Kulingana na wakati wa uhai kwa Sara, nitakuzuru tena, nawe utamzaa mtoto huyo mchanga."

226 Naye Sara, nyuma Yake, hemani, vifuniko vimefungwa, alicheka moyoni. Hivi tu. . . [Ndugu Branham anaiga kicheko kimya—Mh.] Naye akasema moyoni mwake, "Ningeweza kuwa na raha pamoja na bwana wangu?" Unamwitaje mume wako? "Nitapata raha na bwana wangu tena, kwa kuwa mimi ni mkongwe, naye ni mkongwe, pia?"

227 Naye Malaika, akiwa amegeuza mgongo Wake, akasema, "Kwa nini Sara akacheka? Ni kitu gani kilichomfanya acheke?" Hivi hamwoni? Ni Roho ya aina gani, ni Malaika wa namna gani, huyo, aliyelitembelea Kanisa hilo teule kule?

228 Sasa, Yesu alisema ya kwamba jambo lilo hilo litatukia kabla tu ya Kuja Kwake. Hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Kuja Kwake.

229 Hebu tuitishe mstari wa maombi. Yeye alifanya ahadi. Yeye anaitimiza. Sasa, hapo, mahali fulani pale, sina budi kuita watu watano ama sita, wote wanaoweza kusimama hapa. Ninyi wengine nyote aminini tu. Tazameni. Endapo huna kadi ya maombi upate kuja huku, hilo halimaanishi kitu. Nawapa changamoto. Hili hapa lile. . .

230 Hivi ndivyo yule Mzao wa Ibrahimu alivyofanya, Yesu, alipokuwa duniani.

231 Siku moja, Yeye alikuwa akipitia kwenye umati wa watu. Nao hao wote walikuwa wakisema, "Aloo, Rabi. Habari za asubuhi, Daktari. U hali gani, Kasisi? Nina furaha kukutana na Wewe, Kasisi. Nina furaha kuwa Nawe hapa. Utafanya mkutano wakati tukiwa huku?"

232 Basi maskini mwanamke mmoja alikuwa na haja, kwa hiyo akaingia kisiri kwenye umati na kugusa vazi Lake. Kwa

kuwa alisema moyoni mwake, “Kama nitamgusa tu yule Mtu mtakatifu.” Mnaona? Imani yake. Mnaona? “Kama nikimgusa, nitapata afya.” Kwa hiyo akamgusa, kisha akarudi kwenye umati. Akasema, “Loo, nina hakika nimeponywa, kwa sababu ninaamini hilo. Nililiamini. Ninajua nimeponywa. Na—naamini tu kutokwa na damu kunakoma sasa hivi. Ninaamini tu.”

233 Yesu akasimama, kasema, “Aisee, ni nani aliyenigusa?” Ni swali la namna gani!

234 Petro akasema, kwa maneno mengine, “Bwana, una shida gani Wewe?” Biblia ilisema alimkemea. Kasema, “Unamaanisha nini kwa hilo? Mbona, kila mtu anakugusa! Kwa nini unafikia kusema. . .Wewe, ukiwa ni Masihi, hivi huogopi utajianika Mwenyewe hapa mbele ya watu hawa, ‘Ati ni nani aliyenigusa?’ Nami nina hakika kumekuwako na watu mia tano waliokugusa katika hii dakika moja ya mwisho. Ungesemaje, kitu kama hicho?”

235 Akasema, “Lakini huu ulikuwa ni mguso wa tofauti. Naona nimekuwa dhaifu.” Nguvu, mtu yeyote anajua nguvu ni uweza. “Nimekuwa dhaifu. Nguvu zimenitoka.”

236 Naye akaangalia kote, akaangalia kote. Mnaona, kuna imani huko nje, mahali fulani. Akaangalia kote, ndipo akampata maskini mwanamke huyo. Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani Yake, katika utimilifu, akamwongoza moja kwa moja kwa maskini mwanamke huyo. Huko kutokwa na damu alikokuwa nako, Yeye alisema, “Imani yako! Sasa, kamwe sikukuponya. Kamwe sikuwa na uhusiano wowote nalo, bali imani yako,” (katika Nani?) “katika Mungu, Yule ninayemwakilisha, imani yako imekuponya.”

237 Sasa, Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kusema, yeye yule katika kanuni, yeye yule katika nguvu, yeye yule katika mtazamo. Mungu yeye yule aliyeishi katika Kristo, anaishi katika Kanisa, sio kiasi kama Chake. Yeye alikuwa naye pasipo kipimo, sisi tunaye kwa kipimo. Lakini kama ungalikuwa na maji kijiko kimoja, kutoka baharini, kemikali zile zile zilizokuwa kwenye bahari nzima, zimo kwenye hicho kijiko kimoja. Kumbukeni hilo. Hiyo ni kweli. Ni Mungu yule yule.

238 Sasa, Biblia ilisema, katika Waebrania, Yeye alisema kwamba, “Yesu Kristo sasa hivi ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Ni wangapi wanajua hilo? Vema, iwapo Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule, hivi si angetenda vile vile kama akiguswa?

239 Sisi ni nini? Msemaji Wake. Tunajitolea Kwake, nayo maneno yetu si maneno yetu. “Usiwazie utakayosema, maana si wewe unayenena. Ni Baba anayeishi ndani yako. Yeye hunena.”

240 Mahali fulani, palikuwa ni wapi, Billy, moja hadi hamsini, ama moja hadi mia moja? [Ndugu Billy Paul anasema, “Mia moja.”—Mh.] Moja hadi mia moja.

241 Kwa kawaida, watu hukimbilia kadi hiyo ya kwanza, kwa hiyo tutaiacha hiyo kwa dakika moja. Hebu tuanzie kwenye namba ya ajabu ajabu, tuseme, thelathini. Ni nani aliye na kadi ya maombi thelathini? Inua mkono wako.

242 He—herufu ni ipi? [Ndugu Billy Paul anasema, “B.”—Mh.] B, B thelathini. Vema.

243 Angalieni mifukoni mwenu, toa kadi yako ya maombi. Na iwapo kuna. . . [Ndugu mmoja anasema, “Pale pale.”—Mh.] Vema, sikilizeni, iwapo hamna thelathini, mbona, tutaanzia mahali pengine basi. Tuta—tutaanzia kwenye. . . [Ndugu Billy Paul anasema, “Pale pale, nyuma.”] Wasemaje? [Ndugu Neville anasema, “Yule pale.” Ndugu Billy Paul anasema, “Nyuma, upande wa kushoto.”] Loo, samahani. Samahani. Vema. Njoo hapa, bwana.

244 Thelathini na moja. Ni nani aliye na kadi ya maombi thelathini na moja, waweza kuinua mkono wako? Thelathini na moja. Njoo papa hapa, bwana. Thelathini na mbili. Ni nani aliye na kadi ya maombi thelathini na mbili? Wewe, msichana? Thelathini na tatu. Ni nani aliye na kadi ya maombi thelathini na tatu? Waweza kuinua mkono wako? Mama huyu, hapa. Vema, dada. Thelathini na tatu. Thelathini na nne. Kwa kadi ya maombi thelathini na nne? Wewe, bwana? Thelathini na tano. Thelathini na sita. Thelathini na sita. Ni nani aliye na kadi ya maombi thelathini na sita? Niliikosa?

Una thelathini na sita, msichana? Thelathini na saba. Mama huyu alichanganyikiwa hapa. Tafuta kujua. . . Namba ya kadi yako ya maombi ni ipi? Angalia mahali alipo. [Dada huyo anasema, “thelathini na tano.”—Mh.] Thelathini na tano. Samahani, mama. Vema, chukua mahali pako. Hao wavulana hapo watakuweka mahali unapopaswa kuwa.

Thelathini na saba, thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini. Hebu tuwaone wakisimama. Wako watatu sasa. Thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini. Thelathini na tisa, arobaini. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba nane, tisa, nadhani ni hao tu. Arobaini, arobaini na moja, arobaini na mbili, arobaini na tatu, arobaini na nne, arobaini na tano. Hebu hizo kadi za maombi zije huku: kadi ya maombi, hadi arobaini na tano, kuanzia thelathini hadi arobaini na tano.

Sasa, kama huwezi kusimama. . . Una kadi ya maombi, bwana? Unayo, vema, nenda pale. Sioni ila mtu mmoja kiwete. Ameketi hapa kwenye kiti cha magurudumu. Sasa, kama kuna yeyote asiye na hizo kadi za maombi, sasa, hatujui. . . Nadhani ninapata msongamano hapo, kwa hiyo mimi. . . Sawa. Vema.

Nita—nita—nitasimama, katika dakika moja tu. Vema. Hatuna nafasi hapa, mnaona, kufanya yote kwa utaratibu.

245 Sasa, ni wangapi humu ndani wasio na kadi ya maombi, na hata hivyo, wewe ni mgonjwa, na unataka Mungu akuponye? Inua mkono wako. Vema, ni karibu kila mahali, nadhani, karibu tu kila mahali.

Vema, sasa, nitawauliza, mkiweza, kwa dakika hizi zingine chache zifuatazo. . . Ambapo, nimechukua wakati wangu sasa.

Lakini, hili hapa shindano la kuamua kama Neno hili ni la kweli au la! Hili linalithibitisha!

Sasa, hebu nipate usikivu wenu mkamilifu.

Mtu yeyote hapa anajua, kwamba, kama ningaliweza, ningemponya kila mmoja wenu. Lakini Biblia ilisema, ya kwamba, "Mimi ndimi Bwana Mungu wako akuponyaye magonjwa yako yote." Imewekwa msingi juu ya Imani. Mambo haya yote ambayo nimehubiri juma hili, kufikia wakati huu, na kote maishani mwangu, yamewekwa msingi juu ya kazi zilizomalizika za Kristo pale Kalvari. Kama unaamini hilo, hilo tu ndilo Mungu aombalo: "Kama utaamini, yatakuwa yako uliyoomba."

Sasa, kuhusu ishara na maajabu kutokea, Yeye aliahidi hilo. Kwanza, Yeye aliweka kanisani (Nini?) mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, wachungaji. Huo ndio utaratibu wa Mungu uliowekwa kanisani, kuwakamilisha watakatifu.

Sasa, ninamtaka kila mmoja wenu kunipa usikivu wenu mkamilifu.

Sasa, kuna yapata mtu mmoja tu kwenye mstari ule wa maombi ambaye ninafikiri ninamjua. Na huyo ni yule mtu aliyevaa suti nyeupe. Siwezi kulikumbuka jina lake. Lakini na—naamini ametoka mahali fulani, yapata, huko juu karibu na Carolina, ama kitu kama hicho. Mimi. . . Yeye ni muuza magari ama kitu fulani. Nimezungumza naye. Hata sijui jina lake. Lakini mimi. . . Na kwa kweli, si—sijui yeye ana shida gani. Mimi. . . Mungu anajua hilo. Nisingejua yuna shida gani. Lakini nafikiri hao wengine wote hatufahamiani. Siwajui.

246 Ni wangapi hapa nje wanaojua sijui lolote kuwahusu? Inueni mikono yenu. Naam, bwana. Sasa, Biblia ilisema, "Roho Mtakatifu atakapokuja, Yeye ataninii. . ." (Jambo la kwanza, Roho Mtakatifu atafanya nini?) ". . . kuwafunulia mambo haya, niliyowafundisha." Hiyo ni kweli? Basi Yeye angefanya nini? "Kuwapasha habari za mambo yajayo, awe Mfunuzi wa siri za moyo." Angefanya kazi zile zile ambazo Yesu alifanya.

247 Sasa, ni wangapi wanaamini ya kwamba Yesu alikamilisha mpango wa wokovu na uponyaji, pale Kalvari? Hakika. Kwa hiyo, kuhusu hilo, yote yamekwisha, sivyo? Yote yamekwisha.

248 Lakini jambo pekee analoweza kufanya ni kukushtusha, ama kukuleta kwenye ufahamu ya kwamba Yeye angali ni Mungu na hutimiza ahadi Yake. Kwa hiyo, katika kufanya hivyo, Yeye anawapaka mafuta wahubiri. Hao ni hawa watu wazuri wanaosimama hapa, na wengi huko nyuma. Yeye huwapaka mafuta kuhubiri. Mimi ni kibadala duni cha mhubiri. Yeye alinipa *hiki*, kwa ajili ya kuhubiri kwangu, mnaona, badala yake. Maana, sina elimu wala sijui chochote, mnajua ninalomaanisha, kuwa mwanachuoni ama chochote kile, ama mwanafunzi. Lakini amewapa watu hawa nafasi ya kufanya hilo, nao wanasimama pale chini ya upako na kuhubiri. Loo, wangeweza kusema mengi katika dakika tano kuliko ningaliweza kusema katika saa moja, kwa sababu, chini ya upako, kama tu mzinga ama bombomu ikipiga upesi sana moja kwa moja, kama nyundo ya kushindilia ikipiga. Mnaona?

249 Mimi, mnaona karama yangu ni kitu kingine: inanilazimu kuchukua wakati wangu na kuchunguza yale. . .na kungojea nione yale Roho Mtakatifu ataniambia tena. Na kuona, si hasa katika mkondo wangu. Lakini hata hivyo ninafanya hivyo, kusudi nilijenge kusanyiko, kuwafahamisha kwamba dhana yangu ya Kristo ni nini.

Kwa kawaida katika mikutano, nina mhubiri mzuri kuhubiri kwa niaba yangu. Lakini sasa, huu ndio wakati; hii ndiyo saa, baada ya Neno kuhubiriwa: Basi vipi kuhusu hilo? Kama ni kuhubiri tu, unaondoka, vema, hujui. Lakini kama Yeye akija huku, na kuthibitisha ya kwamba yale aliyosema Yeye ni Kweli, basi, ndugu, ni juu yako, basi. Hiyo ni kweli, ni wewe.

Sasa, kama Roho Mtakatifu atakuja asubuhi ya leo kwenye hili kusanyiko, na kufanya jinsi hasa Yeye alivyofanya alipokuwa katika Yesu Kristo, ni wangapi hapa ndani wataamini ya kwamba Mungu wakati mmoja alikuwa juu yetu; kisha pamoja nasi, katika Kristo; sasa ndani yetu, katika Kanisa? Hakika.

Sasa, kama unaweza kuona sasa, haikubidi kuwekewa mikono, kama wewe ni mwaminio halisi. "Wakati Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu aliwashukia." Mnaona? "Sihitaji, uje ukaweke mikono yako juu ya mtumishi wangu: sema tu Neno, na hilo tu ndilo unalopaswa kufanya." Angalia kama wewe ni mzao wa Ibrahimu sasa. Acha Mungu afanye yaliyosalia.

Baba wa Mbinguni, kama mwanadamu, kama mtumishi, hilo ni neno langu lililomalizika. Wewe nena kutoka hapa na kuendelea, Bwana. Na iwe hivyo, kwamba watajua ya kwamba Wewe ni Mungu katikati ya watu. Katika Jina la Yesu, Amina.

250 Sasa, kama mwanadamu, huyu hapa mtu kama tu, vema, ningesema, ya kwamba, wakati Nathanaeli alipokuja mbele ya Yesu. Nijuavyo mimi, hatujapata kukutana; sisi hatufahamiani. Lakini Mungu anamjua huyu mtu, simjui mimi. Katika

kumbukumbu yangu sijawahi kumwona, isipokuwa iwe tu ni mtaani mahali fulani, na nikakutana naye huko nje, nikampa mkono, ama kusema, “U hali gani, bwana?” ama kitu kama hicho, asubuhi moja, ndiyo tu nijuayo. Lakini Mungu anamfahamu huyu mtu. Sasa, iwapo Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi Yeye ameninii . . . endapo mtu huyu ni mgonjwa, basi, kuhusu uponyaji, Yeye tayari ameufanya. Yesu tayari ameumaliza huo. Lakini njia tu ya kumfanya, aamini, kujua ya kwamba Yesu yuko papa hapa.

251 Sasa Yesu alisema nini? “Ile ishara, kama ilivyokuwa huko Sodoma, ndivyo itakavyofanywa katika siku za mwisho.” “Kazi nizifanyazo,” ikionyesha ya kwamba alikuwa ni Yeye yule aliyekuwa pamoja na Ibrahimu. “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Yeye alikuwa Malaika yule. Na hapa Yeye . . . Yeye huyu hapa, hapa asubuhi ya leo, Malaika yeye yule, akiishi ndani yetu.

252 Sasa, mtu huyu huenda akawa mwi—mwigaji. Huenda akawa ni mnafiki. Huenda akawa ni kafiri. Huenda akawa ni m—mtakatifu. Yeye, sijui lolote kumhusu. Yeye amesimama hapo tu. Lakini kama Roho Mtakatifu atakuja na kufunua, kwake, na awe hakimu tangu hapo na kuendelea. Yeye anajua. Iwapo Roho Mtakatifu anaweza kumwambia yale yamekuwa katika maisha yake, hakika yeye, kama hiyo ni kweli, angeweza kuamini yale yatakayokuwa maishani mwake. Hiyo ni kweli? Kama angeweza kusema yale yamekuwako, na yatakayokuja je? Sasa, yeye atajua kama ni kweli ama si kweli, kama imekuwa.

253 Daktari, wewe amini hili. Wewe na mama, nyote wawili, aminini. Na yule daktari mwingine anayeketi kule nyuma, pia, kutoka Springfield, Missouri. Mnaona? Roho Mtakatifu yuko humu ndani sasa.

254 Mtu mwenye mvi hapa, anayekaa kwenye Moteli ya Alben hapa nje. Unaumwa na kitu fulani ubavuni mwako. Hutoki hapa, kwanza kabisa. Umetoka Canada. British Columbia. Vancouver. Umetoka Finland. Kiitos.

255 [Ndugu huyo anasema, “Kiitos, na Mungu akubariki.”—Mh.] Mungu akubariki. Nenda nyumbani; umepona. Yesu Kristo anakuponya.

256 Unaamini? Simjui huyu mtu. Sijui sasa yale niliyomwambia. Huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu akizungumza.

257 Mgeni mwingine. Simjui mtu huyu, sijawahi kumwona maishani mwangu. Nadhani hatufahamiani. Hiyo ni kweli, bwana? [Ndugu huyo anasema, “Kweli. Hiyo ni kweli.”—Mh.]

258 Sijawahi kumwona huyu mtu, sijui lolote kumhusu. Sasa iweni na kicho kabisa. Na endapo sijui lolote kumhusu huyu mtu, naye Bwana ataniambia jambo fulani kumhusu, basi hakika hilo lingethibitisha ya kwamba inahitaji kitu fulani zaidi ya mwanadamu kufanya hivyo. Sivyo? Sasa kama mtakuwa na uchaji kweli, na kuangalia, na kuwa waangalifu. Ndipo

wakati Roho Mtakatifu anaponong'oneza juu yako namna hiyo, umkubali. Mwamini, kwa moyo wako wote.

259 Mgeni. Jambo la kwanza, unatafuta wokovu. Wewe ni mlevi sugu. Hiyo ni kweli kabisa. Hutoki kwenye mji huu. Umetoka mji mwingine, mji wa Indiana. Naam. Ninaamini ni New Castle, kitu kama hicho. Hiyo ni kweli kabisa. Um-hum.

260 Uko pamoja na, *kwa njia nyingine*, ninaona mtu fulani... uko pamoja na mwanamke, inahusiana...Yuko wapi Lyle Woods? Ni mkewe. Yeye yuko hapa sasa. Anataka kuombewa, pia. Naam, bwana. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Ugonjwa wa moyo. Ataamini kwa moyo wake wote, anaweza kuponywa.

261 Ninamhukumu ibilisi huyo ndani yako, anayekufanya kunywa pombe. Nenda nyumbani, katika Jina la Yesu Kristo, na usinywe pombe tena. Batizwa katika Jina Lake la thamani, ukaondelewe mbali dhambi. Nami namhukumu huyo ibilisi, naomba aondoke kwako. Amina.

262 Endelea. Mungu akubariki, bwana. Dhambi zako zimesamehewa sasa. Nenda zako, na usitende dhambi tena.

263 Mwamini Mungu. Usitie shaka. Amini kwa yote yaliyo ndani yako.

264 Hatufahamiani, ewe msichana. Unaamini Kristo anatujua sote wawili? Hii ni kama yule mwanamke kisimani, na Mwokozi wetu. Wewe siye, wala mimi si Yeye. Bali Roho Yake inaishi milele. Huyu mwanamke, msichana huyu anayesimama hapa, ana...Kama mngeweza kumwona, kati yake na mimi kuna Nuru hii ya Malaika aliyesimama hapa. Lakini kupita tu hapo kuna kivuli, nacho kivuli hicho ni mauti, giza. Ni kansa. Hiyo kansa iko, kwenye rektamu. Hutoki katika nchi hii, pia. Wewe ni Mkentaki. Kutoka LaGrange, Kentaki. Hiyo ni kweli. Binti Johnson, hebu nikwambie. Kama unaamini, kwa moyo wako wote, rudi nyumbani, na Yesu Kristo anakuponya. Unaamini hilo? [Dada Johnson anasema, "Ninaamini."—Mh.]

265 Ninamhukumu ibilisi anayeyachukua maisha ya mwanamke huyu. Juu ya msingi wa kufufuka kwake Yesu Kristo, sasa ninampa Shetani changamoto, na kumwambia ya kwamba yeye ni kiumbe kilichoshindwa, kwamba Yesu Kristo alimshinda pale Kalvari. Na kama mtumishi wa Mungu, chini ya upako wa Roho Mtakatifu, kwamba, lile agizo nililopewa na Malaika, ninamhukumu ibilisi huyu, kwa ajili ya maisha ya mwanamke huyu. Jalia aishi, Ee Bwana. Amina.

266 Rudi nyumbani, shangilia na uwe na furaha, ukimshukuru Bwana. Usiwe na shaka sasa. Usiwe na shaka niani mwako.

267 Unaonekana mwaminifu mno na asiye na hatia kuhusu hilo, mama. Kama ukiamini, ugonjwa huo wa tezi unaougua, yabisi kavu, amini kwa moyo wako wote, utakuacha.

268 Sasa maskini mama huyo alihisi kitu Fulani papa hapa, maana kuna roho fulani kati yao wawili, mnaona. Wewe, yako ni sawa, pia. Amini tu, kwa moyo wako wote.

269 Na jambo lingine, maskini mama huyo karibu naye hapo. Naam, huyo ni wewe unayeketi hapo, ukiangalia juu, ukiomba. Uh-huh. Ugonjwa huo wa mgongo, amini kwa moyo wako wote. Na wewe, pia, ulikuwa na ugonjwa wa moyo, pia. Kwa hiyo panda tu uende nyumbani sasa, uwe mzima.

270 Unaamini, kwa moyo wako wote? Uko hapa kwa ajili ya binti yako. Binti yako ametiwa uvuli wa mauti. Ni kansa. Nayo hali yake ya kiroho si nzuri sana. Naam, bwana. Yeye yuko tu juu-chini, kuingia na kutoka, na kutangatanga. Unaona leso hiyo uliyo nayo mkononi mwako? [Dada huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Unaamini kwamba huyo ni Roho Mtakatifu anayezungumza hapa? ["Ninaamini."] Naomba unipe hiyo leso.

271 Bwana, katika Jina La Yesu Kristo, ninauhukumu ugonjwa wa binti yake. Juu ya maneno ya mama yake, na itende kazi juu yake, katika Jina la Yesu. Amina.

272 Nenda; usitie shaka. Kuwa na imani. Anaweza kwenda nyumbani sasa. Weka leso hiyo juu yake. Amini. Mwamini Mungu.

273 Kunaye mwanamke, endapo mnaweza kumwona. Ameyafunga macho yake. Leso yake juu, akiomba, akiyapangusa macho yake. Uligusa kitu Fulani, dada. Hukunigusa mimi, bali ulimgusa Yeye. Sasa, una mishipa iiliyovimba, tatizo la kike, magonjwa ya ziada ya kila namna. Hiyo ni kweli, sivyo? Inua mkono wako iwapo hiyo ni kweli. Vema. Sasa nenda nyumbani, upate afya.

274 Aligusa nini? Ninataka kuwaulizeni. Ni nani, mwanamke huyo aligusa nini? Kuhani Mkuu. Mnaweza kutambua? Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yuko hapa. "Kama unaweza kuamini!"

275 Huyo Roho yuko kwenye kusanyiko. Iweni mkiamini. Nguzo ile ya Moto iliyomo kwenye picha hii hapa, inatembea kwenye kusanyiko. Ni mwanamke anayeniangalia moja kwa moja. Inasimama juu yake. Mikono juu namna *hii*, pamoja na leso kinywani mwake. Yuna maumivu kichwani mwake, kidogo ni ugonjwa wa mishipa ya kichwani. Hiyo ni kweli. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaamini huyo kuwa ni Kristo anayekuzungumzia? Nenda nyumbani, utapata afya. Amini kwa moyo wako wote.

276 Mtu anayeketi papo hapo nyuma yake, kitu fulani kiliungana naye kuhusu Campbellsville, Kentucky. Uh-huh. Una ugonjwa wa mishipa, pia; tezi dume; shinikizo kuu la damu. Unaamini kwa moyo wako wote, bwana? Iwapo unaamini, inua mkono wako endapo mambo hayo ni ya kweli. Uligusa kitu gani?

Ulimgusa mtu Fulani, Kuhani Mkuu. Nenda, uamini, na upate afya.

277 Huyu hapa mwanamke, kidogo ni mnene, ameketi hapa ameinua mkono wake karibu naye. Ninaamini ninamfahamu mwanamke huyo. Nimeshamwona mahali fulani. Yeye anaomba. Ana maumivu kichwani mwake. Na mara niliposema "kichwa," kwa mwanamke huyo mwingine, dakika chache tu zilizopita, lilimgusa. Yuna maumivu ya kichwa, pia. Nimemwona huyu mwanamke mahali fulani. Siwezi kumkumbuka, lakini nimemwona. Loo, naam, nakumbuka. Ninajua sasa, hata kiroho. Yeye ni Rose Austin, kutoka Louisville, Kentucky. Amini sasa. Nenda zako nyumbani, upate afya.

278 Ninakujua. Ninajua ninii wako. . .Ninaujua uso wako. Nilikuwa pamoja nawe, katika ma—mahojiano, kwenye trela, ambako ulimpokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Nikakuwekea mikono, na ukapokea. Sijui jina lako ni nani sasa hivi, bali ninakujua. Una biashara ya magari. Hayo tu ndiyo nijuayo. Sina fununu una shida gani. Wewe, unajua hilo. Hiyo ni kweli. Sina fununu. Iwapo Mungu atafunua shida ni nini, basi Yeye yule aliyekupa Roho Mtakatifu, anaweza kukuponya, akupe shauku ya moyo wako. Unaamini hilo? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Sio ugonjwa wako. Ni kwa ajili ya mpendwa. Ni dada huko Virginia. Tatizo la namna fulani, kama mgongo.

279 Mke wako ameketi pale. Yeye pia ni mhitaji. Angeamini, maskini huo ugonjwa wa moyo na kadhalika utamwacha tu. Ataninii. . .

280 Mwanamke huyu papa hapa ana uhusiano nawe. Huyo ni mama yako. Anasumbuka kama yuna Roho Mtakatifu, ama hana. Pia, ana ugonjwa wa kibofu unaomsumbua, na kitu kingine. Daktari pale, kidogo ni jamaa mwenye nguvu, alisema, "Ni tumbo la uzazi lililoanguka." Ulipaswa kufanyiwa upasuaji, wakati fulani uliopita. *Yeye* alikuwa ndiye chanzo cha wewe kutokufanyiwa upasuaji. Alitaka uje hapa ukaombewe.

281 Yule anayesimama papo hapo nyuma yake ni wa jamaa. Msichana huyo ni wa jamaa, kwa namna fulani, bali ni kwa ndoa tu. Mpwa, kwa ndoa. Anasumbuka juu ya wokovu wake, pia. Hiyo ni kweli. Naye ana kisukari, msichana mdogo. Kweli kabisa. Unaamini? [Dada huyo anasema, "Loo, naam, bwana."—Mh.]

282 Hebu tumwinulie tu Mungu mikono yetu.

283 Ee Bwana, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uhai, Mpaji wa kila kipawa chema, utume Uwepo Wako miongoni mwa hawa watu sasa. Wape shauku ya mioyo yao, Bwana. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili. Tukiomba ya kwamba Wewe utabariki tu na kuwapa watu hawa wanachohitaji, kupitia kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

Ni wangapi wanaoamini?

284 Sikumbuki. Lakini, kwa namna fulani, Hiyo ilishuka kupitia kwa laini hii, juu ya mtu fulani. Yote yalikuwa ni kweli? Inueni mikono yenu. Yeyote iliyemzungumzia, ilikuwa ni kweli? Yote ni kweli. Basi, ni kweli kwamba Roho Mtakatifu yuko hapa. Hiyo ni kweli? Sasa niaminini, kama mtumishi Wake. Ninajua ninii... Hamtulii. Mmechoka. Mnaona? Msitie shaka. Aminini sasa ya kwamba huyu ni Yeye. Huo upepo unaoenda kasi uliokuja kwenye Siku ya Pentekoste, katika chumba cha juu, hicho ni kitu kile kile kilichowagusa watu hawa wakati hilo lilipotukia, kwa sababu ni Roho Mtakatifu yule yule. Anazungukazunguka, juu yenu, kila mmoja, sasa hivi. Nje, miongoni mwa umati, ni Roho Mtakatifu akitembea miongoni mwenu.

285 Ni wangapi...? Ninataka mwe waaminifu kwangu, kama vile ingekuwa pamoja na Biblia hii mbele yangu. Ni wangapi wanaohisi hisia ya ajabu kweli, kana kwamba kitu Fulani ndio kwanza kije huku? Huyo ni Roho Mtakatifu. Huyo ni Yeye. Sasa niaminini mimi. Maneno yangu ni ya kweli. Maana, Mungu alithibitisha Kweli Yake kwa Biblia, akaithibitisha kwa Nguvu za kufufuka Kwake, akaithibitisha kwa utafiti wa sayansi, basi hakuna kitu kingine cha kuithibitishia. Yeye ni Mungu. Iko hapa. Basi, nisikieni mimi. Ninawaambia Ukweli. Kila mmoja wenu yuko Mbele za Mungu sasa hivi, kuponywa, kundi lote lenu. Mnaamini hilo?

286 Sasa nawaambia yale ninayotaka mfanye. Ninawatakeni tu, popote mlipo, kila mmoja wenu aweke mikono mmoja juu ya mwenzake, ili kwamba mtaona sio mimi. Mna—mna matokeo yale yale. Wewe ni mwaminio. Kama ukimhisi huyo Roho Mtakatifu...Yuko juu yako, labda sio katika karama kama hii, lakini huyo Roho Mtakatifu yuko juu yako. Mtu fulani, haidhuru ni kitu gani, weka mikono juu ya mtu fulani, kisha uinamishe kichwa chako. Weka mikono yako juu ya mtu fulani, na uinamishe kichwa chako. Ninajisikia kuongozwa kufanya hivi. Ninajisikia kwamba wakati wa uponyaji wenu umewadia. “Kama unaweza kuamini!”

287 Loo, Roho Mtakatifu anatembea juu ya hili kusanyiko! Maskini jamaa yule pale, kutoka Georgia, unayemwombea ndugu yako anayeketi kule nyuma; kuwa na imani, amini. Loo, Yuko kila mahali tu, kila mahali tu.

288 Sasa, usijiombee mwenyewe. Mwombee mtu uliyemwekea mikono. Hilo litamfanya kila mmoja wenu kuomba mmoja kwa mwenzake.

289 Sasa, Bwana Yesu, Mwana wa Mungu, Yule aliyefufuka katika wafu, hata vitisho vya Pontio Pilato na muhuri wa serikali ya Kirumi visingeweza kukushikilia kaburini. Mwenyezi Mungu alishuka kwenye siku ya Pasaka, akalibingirisha lile jiwe, akauvunja ule muhuri. Nawe ulifufuka na ukawa

pamoja na wanafunzi Wako, siku arobaini, ukawaagiza waende ulimwenguni na kufanya mambo haya yanayofanywa sasa. Hiyo imekuwa miaka elfu mbili iliyopita.

290 Bwana, Wewe ni Mungu. Huwezi kushindwa. Uko hapa. Kongamano hili, asubuhi ya leo, ambalo tumekuwa nalo, tumeshauriana pamoja kuhusu mambo haya. Tumetoa hoja kwamba Wewe ni Mungu; tukahojiana, sababu ya Wewe kuwa ni Mungu, na sababu ya Wewe kuwa hapa.

291 Na sasa tuna agizo kutoka Kwako, kuwekeana mikono. Hivyo ndivyo ulivyotuagiza kufanya. Wewe ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hilo ndilo agizo letu kutoka kwenye kongamano. Sasa, Bwana, "Kutii ni bora kuliko sadaka; kusikia, kuliko mafuta ya kondoo dume."

292 Sasa, Bwana, kama mtumishi Wako, ninaagiza, na kumwamuru kila ibilisi, kila pepo, kila maradhi, kila mateso, kila kitu kinyume kinachowasumbua watu hawa. Mbele za Mungu, kwa ushuhuda wa Roho Mtakatifu, kwa agizo la Malaika aliyetumwa kwangu, ninampa pepo huyu changamoto, kwa Neno la Mungu.

293 Roho huyu wa magonjwa na mateso, toka ndani ya hawa watu, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, na uwaache wawe wazima. Waachilie. Shetani, wewe ni laghai tu. Tumekupa changamoto. Wakati umewadia, ambapo Yesu Kristo amejidhihirisha Mwenyewe mbele ya Mataifa. Sasa, Shetani, umeshindwa. Wakati mmoja, uliwashikilia watu. Huna haki za kisheria sasa. Yesu Kristo alikunyang'anya kila haki uliyokuwa nayo, pale Kalvari. Yeye alilipa gharama yote, na kusema, "Imekwisha." Kila, mpango mkamilifu wa wokovu, uponyaji wote, yote yalikwisha pale Kalvari. Nawe, yalitolewa kwako, kila kitu ulichomiliki wakati mmoja, kupitia kwa dhambi na kupitia kwa kule kuanguka. Sasa tumekombolewa na Damu ya Yesu. Wala huwezi kutushikilia tena. Tunasema, "Tuache, katika Jina la Bwana Yesu Kristo."

294 Sasa, endeleeni kuwekeana mikono. Endeleeni kuomba. Endeleeni kuweka mikono yenu. . .Endeleeni kuomba. Kila mmoja wenu akiwazia tu, "Mungu yuko karibu. Roho wa Mungu yuko hapa. Mungu ananiponya. Uzuri Wake, rehema Zake, wema Wake, ahadi Yake inafanywa halisi ndani yangu."

Tungeweza kuendelea kuhubiri kwa majuma kadha wa kadha. Isingeleta tofauti yoyote sasa; Roho Mtakatifu yuko hapa. Hayo tu ndiyo angaliweza kufanya wakati wowote, awe papa hapa sasa.

"Sasa hivi ninaamini Roho Mtakatifu amedhihirishwa kwangu, akinithibitishia ya kwamba Mungu yuko hapa. Ninamwamini. Ni kazi iliyomalizika. Ninayo. Ni mali yangu. Sasa ninajazwa na Roho Mtakatifu. Magonjwa yangu,

maumivu yangu na uchungu yanaondoka. Mateso yangu yote yananiondokea." Hiyo ndiyo njia ya kuwa ukiomba, huku kichwa chako kimeinamishwa, macho yamefumbwa. *(Amini Tu*, sasa.)

295 Endeleeni kuviinamisha vichwa vyenu sasa. Tutaimba sasa, kwa utulivu tu.

Amini tu . . .

296 Akishuka kutoka mlimani . . . Mtoto mwenye kifafa . . . Wanafunzi walikuwa kule, wakishauriana na baba. Yule baba akamkimbilia Yesu, na kusema, "Bwana, msaidie mtoto wangu." Akasema, "Ninaweza, kama ukiamini." "Ninaweza, kama utaamini." Hivyo ndivyo anavyosema sasa: "Niko hapa. Ndio kwanza nishuke kutoka Utukufuni. Niko hapa, niko miongoni mwenu. Ninafanya kongamano hili pamoja nanyi. Nilimtia mchungaji mafuta. Niko hapa. Ninaweza, kama ukiamini."

Kwa kuwa mambo yote yanawezekana, amini tu;
Amini tu, tu . . .

59-1220M Kongamano Pamoja Na Mungu
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org